# KUCHUNGUZA DHAMIRA ZA NYIMBO ZA UGANGA KATIKA JAMII ZA WASWAHILI WILAYA YA MKOANI KUSINI PEMBA

**MUSSA YUSSUF ALI**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA IKIWA NI SEHEMU YA MASHARTI YA KUPATIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI (FASIHI) YA CHUO KIKUU HURIA TANZANIA**

**2016**

**UTHIBITISHO**

Aliyesaini hapo chini anathibitisha kwamba ameisoma na anapendekeza tasnifu hii inayoitwa "*Kuchunguza Dhamira za Nyimbo za Uganga Katika Jamii za Waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba"* ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa shahada ya Uzamili ya Idara ya Lughawiyya na Taaluma za Kifasihi ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

……………..………………………….

Profesa, Dkt, Sk, Mwl. T.Y.S.M Sengo

(Msimamizi)

………………………….……………

Tarehe

## HAKIMILIKI

Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa namna yoyote ile Tasnifu hii kwa njia yoyote kama vile Kieletroniki, Kurudufu nakala Kurekodi au njia yoyote nyingine bila ya idhini ya Mwandishi au Chuo Kikuu Huria Kwa Niaba.

# TAMKO

Mimi, **Mussa Yussuf Ali,** nathibitisha kuwa hii ni kazi yangu halisi na haijawahi kuwasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada hii au nyingine yoyote.

……………………………..

Sahihi

………………………………….

Tarehe

# TABARUKU

Kazi yangu hii ninaitabaruku kwa wazazi wangu kwa kunijengea msingi imara wa malezi bora.

## SHUKRANI

Niwajibu wetu kutanguliza shukrani kwa Mola ambaye ameniwezesha kwa kunipa uhai, afya, hamu ya kuifanya kazi hii. Vile vile namtakia rehma na amani Mtume wetu Nabii Muhamadi (S.A.W) pamoja na Wafusi wake wema mpaka siku ya kiama (Amiin). Kazi hii ni tokeo la michango na miongozo ya watu wengi sana. Ninawashukuru kwa dhati kabisa wote walionisaidia mpaka kufikia hapa. Ningependa niwataje wote, lakini nitawataja baadhi tu ambao michango na miongozo yao ilijichomoza zaidi.

Profesa, Dkt. Mwalimu, Sheikhe, TSYM Sengo anastahili kuongoza katika orodha hii ya washukuriwa. Huyu ndiye msimamizi wa utafiti wangu. Licha ya kukabiliwa na majukumu mazito ya kitaaluma, ninakiri kuwa alionesha ushirikiano usio kifani kwangu katika maandalizi ya tasnifu hii. Kasi ya ajabu katika kusoma sehemu mbalimbali za tasnifu, ukweli na uthabiti katika kufanya marekebisho, upendo, staha na heshima katika kuniongoza na kunikosoa wakati wote wa utayarishaji wa kazi hii.

Upendo kwa wanafunzi wake na tabia ya kushirikiana nao na kuwahimiza umoja ni miongoni mwa tabia za Profesa huyu, ambae kwa hakika tabia zake hizi zilinisaidia sana kunipa nguvu na kuiinua ari yangu kila nilipoonesha hali ya kukwama kutokana na ugumu wa kazi yenyewe.

Ninaushukuru pia uongozi wa Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kupitia Kurugenzi ya Masomo ya Uzamili kwa kunidahili na kunikubali kufanya utafiti katika eneo husika. Shukrani za ziada zimwendee Mwalimu Bakar Kombo kwa kunishika mkono ili

niweze kukamilisha tasnifu hii muda mwafaka. Pia nawashukuru wanafunzi wezangu kwa mashirikiano yao. Nasema ahsanteni'

Mwisho, napenda nitoe shukrani za dhati zisizo kikomo kwa Bi Mwanaika Madi Mzee kwa kunishauri na kuniongoza katika tasnifu hii kwa kuisoma katika hatua ya awali kabla ya kucharazwa na kuwekwa kwenye maandiko. Namuombea kwa Allah ampe malipo mema duniani na akhera ( AMIIN).

## IKISIRI

Lengo kuu la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza dhamira za nyimbo za Uganga katika jammi za waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba**.** Ili kutimiza lengo hili kuu tulikuwa na madhumuni mahususi matatu ambayo ni kubainisha dhamira zinazopatikana katika nyimbo za uganga, kufafanua undani wa dhamira za nyimbo za uganga zilimo katika jamii ya watu wa Kusini Pemba na kufafanua vipengele vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za uganga. Data za utafiti zimekusanywa kwa kutumia njia ya usaili na njia shirikishi katika maskanini. Data hizo zilikusanywa na kuchambuliwa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Vile vile njia za kimaktaba zilitumika kwa mtafiti kwa ajili ya kujisomea kazi tangulizi na maandiko tafauti kwa lengo la kujiongezea maarifa na kufanikisha utafiti wake. Pia uchambuzi wa data ulifanywa kwa kutumia mkabala wa kinadharia. Nadharia zilizotumika ni Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji. Ama kuhusu matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa kwenye nyimbo za uganga kuna siri ambazo zimejificha na zilihitajika kuwekwa bayana na mtafiti. Kwa upande wa dhamira zilizojitokeza katika nyimbo za uganga zilitoa dhamira kama vile suala la Mmongonyoko wa Maadili, umoja na mshikamano, malezi, matabaka na kadhalika. Mwisho matfiti alitoa hitimisho, mapendekezo ya tafiti nyingine zifanyika katika muktadha wa uganga kwa kuangalia misamiati na njungu katika tiba ya uganga na kuiomba jamii yake iziendeleze tiba za asili katika fani ya uganga.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO** ........ **ii**
**HAKIMILIKI** ........ **iii**
**TAMKO** ........ **iv**
**TABARUKU** ........ **v**
**SHUKRANI** ........ **vi**
**IKISIRI** ........ **viii**
**YALIYOMO** ........ **ix**
**ORODHA YA VIAMBATANISHI** ........ **xiv**
**ORODHA YA VIFUPISHO** ........ **xv**
**SURA YA KWANZA** ........ **1**
**UTANGULIZI KWA UJUMLA** ........ **1**
1.1 Utangulizi ........ 1
I.2 Usuli wa Mada ........ 1
1.3 Sababu ya Kuchagua Mada ........ 3
1.4 Tatizo la Utafiti ........ 3
1.5 Lengo la Utafiti ........ 5
1.6 Madhumuni Mahsusi ........ 5
1.7 Maswali ya Utafiti ........ 5
1.8 Umuhimu wa Utafiti ........ 5
1.9 Vikwazo vya Utafiti ........ 6
1.9.1 Utatuziwa Vikwazo vya Utafiti ........ 6
1.11 Eneo la Utafiti ........ 7

1.12 Hitimisho ........ 7

**SURA YA PILI ........ 8**

**UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........ 8**

2.1 Utangulizi ........ 8

2.2 Maana ya Utalii ........ 8

2.3 Maana ya Mkabala ........ 8

2.4 Maana ya Nyimbo ........ 8

2.4.1 Sifa za Nyimbo ........ 10

2.4.2 Aina za Nyimbo ........ 10

2.4.2 Maana ya Uganga ........ 14

2.4.3 Nyimbo za Uganga ........ 14

2.5 Dhana ya Dhamira ........ 16

2.6 Vipengele vya Kifani ........ 17

2.6.1 Wahusika ........ 17

2.6.2 Mazingira /Mandhari ........ 17

2.6.3 Lugha ........ 17

2.7 Utalii wa kazi Tangulizi ........ 18

2.8 Mkabala wa Kinadharia ........ 21

2.8.1 Maana ya Nadharia ........ 21

2.8.1.1 Nadharia ya Simiotiki ........ 22

2.8.1.1.1 Muhimili wa Kimatukio ........ 24

2.8.1.1.2 Muhimili wa Kiishara ........ 24

2.8.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ........ 25

2.9 Hitimisho ........ 26

**SURA YA TATU ........ 27**

**MBINU ZA UTAFITI ........ 27**

3.1 Utangulizi ........ 27

3.2 Kuteuwa Kundi Lengwa ........ 27

3.3 Uteuzi wa Watafitiwa ........ 27

3.4 Ukusanyaji wa Data ........ 28

3.4.1 Data za Awali (Msingi) ........ 29

3.4.2 Data za Upili ........ 29

3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ........ 30

3.5.1 Mbinu ya Usaili ........ 30

3.5.2 Mbinu Shirikishi ........ 31

3.6 Mbinu za Uchanganuzi wa Data ........ 32

3.7 Vifaa vya Utafiti ........ 32

3.7.1 Kalamu na Karatasi ........ 33

3.7.2 Ngamizi/Kompuyuta ........ 33

3.7.3 Shajara ........ 33

3.7.4 Simu na Kirimbo ........ 33

3.8 Maadili ya Utafiti ........ 34

3.9 Hitimisho ........ 34

**SURA YA NNE ........ 35**

**UWASILISHAJI, UCHAMBUZI, NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI. 35**

4.1 Utangulizi ........ 35

4.2 Uwasilishaji wa Data ........ 36

4.3 Dhamira ya Kusifu mtu au Kitu katika Jamii ........ 38

4.4 Dhamira ya Mmong’onyoko wa Maadili ... 40
4.5 Dhamira ya Umoja na Mshikamano ... 42
4.6 Dhamira ya Kufunza ... 43
4.7 Dhamira ya Matabaka ... 45
4.8 Dhamira ya Malezi ... 46
4.9 Dhamira ya Kuonya ... 48
4.10 Dhamira ya Imani ya Dini ... 49
4.11 Dhamira ya Kuelimisha ... 50
4.12 Dhamira ya Maadili ... 52
4.13 Undani wa Nyimbo za Uganga ... 53
4.13.1 Siri ya Uganga ... 53
4.13.2 Suluhisho ... 55
4.13.3 Undani wa Shukurani ... 57
4.14 Uchambuzi wa Vipengele Vya Kifani ... 58
4.14.1 Mandhari ... 58
4.14.1.1 Mazingira ya Giningi ... 60
4.14.1.2 Mazingira ya Nyumbani ... 60
4.14.1.3 Mazingira ya Baharini na Porini ... 61
4.14.2 Matumizi ya Lugha ... 62
4.14.2.1 Matumizi ya Taswira ... 63
4.14.2.2 Lugha ya Picha ... 64
4.14.2.3 Tashihisi ... 64
4.14.2.4 Matumizi ya Ishara ... 65
4.14.2.5 Chuku/ Mubalagha ... 65

4.14.3 Wahusika........................................................................................................ 66

2.14.3.1 Wahusika Ndege ........................................................................................... 66

4.14.3.2 Muhusika Samaki.......................................................................................... 67

4.15 Hitimisho......................................................................................................... 67

**SURA YA TANO ......................................................................................................... 68**

**HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO......................................... 68**

5.1 Utangulizi ............................................................................................................ 68

5.2 Muhtasari wa Tasnifu........................................................................................ 68

5.3 Matokeo ya Utafiti ............................................................................................ 70

5.4 Mapendekezo ya Utafiti ................................................................................... 71

5.5 Hitimisho............................................................................................................. 71

**MAREJELEO ................................................................................................................ 73**

**VIAMBATANISHI ........................................................................................................ 78**

# ORODHA YA VIAMBATANISHI

Kiambatanishi 1: Mwongozo wa Maswali ya Utafiti wa Maskanini kwa Watafitiwa ........ 78

Kiambatanishi 2: Nyimboza Uganga ........ 80

# ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bi | Bibi |
| Dkt | Daktari |
| M.A | Master of Arts |
| Mw | Maalim |
| Prof. | Profesa |
| S.A.W | Swallallah Alayhi Wasallam |
| Sk | Sheikhe |
| SW | Subhanahu Wataala |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI KWA UJUMLA

## 1.1 Utangulizi

Mada ya utafiti huu ni Kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya Waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba**.** Mada hii iliteuliwa ili kuziba pengo la kiutafiti lililodhihirika baada ya kudurusu kazi tangulizi. Kazi hizo kwa muonekano mkubwa ziligusia nyimbo zikiwemo za uganaga lakini hazikushughulikia dhamira za nyimbo za uganga za wanajamii ya waswahili wa Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba. Hivyo basi, utafiti huu ulishughulikia usuli wa mada, sababu za kuchagua mada, tatizo la utafiti, sambamba na lengo na mahumuni mahususi ya utafiti. Vile vile maswali na umuhimu wa utafiti pamoja na vikwazo vya utafiti, mipaka na eneo ambalo utafiti huu umefanyika ambayo ni Kisiwa Panza, Mkanyageni na Michenzani maeneo hayo yote yapo Wilaya ya Mkoani, Mkoa wa Kusini Pemba.

## I.2 Usuli wa Mada

Mulokozi (1981), anasema kwamba wimbo ni ushairi ambao hutumia sanaa ya lugha, inayoonyesha na kueleza jambo. Senkoro (1988) anasema kuwa nyimbo ni msingi wa maneno yenye hekima tangu kale na ndicho kitu kilicho bora katika maongozi ya dunia, kwa kutumia maneno ya mkato, lugha mzito. Kwa kutumia tafsiri hii ya nyimbo ni wazi kwamba nyimbo zote hujengwa kwa lugha iliyojaa tamathali za semi ili kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Finnegan (1977) na Sengo (1978) wanasema kwamba nyimbo zilianza pale tu binaadamu alipoanza kupambana dhidi ya mazingira yake katika shughuli mbali mbali za uzalishali mali.

Nyimbo za uganga zinahusishwa na uponyeshaji wa wagonjwa kwa kuwapa dawa. Vile vile, nyimbo za uganga ni aina ya nyimbo zinazowasilishwa na waganga kwa wanajamii kwa lengo la kutolea tiba katika shughuli hiyo na kufikisha ujumbe kwa wanakilinge na jamii kwa ujumla. Mganga hutoa au huimba nyimbo kwa lengo la kumwita shetani ili aweze kuelewana naye katika kilinge, lakini kiuhalisia huwa anatoa ujumbe kwa hadhira yake. Uganga ni elimu kuhusu tiba za magonjwa ya watu, wanyama, mimea, mwilini na rohoni jinsi ya kuzuia magonjwa na kuhusu njia ya kurudisha uzima. (SW.wikipedia.org/wiki/Tiba). Ibnu Bazi (1982) ametoa hoja isemayo kwamba, uganga ni fani au taaluma au elimu ambayo watu huitumia kutibu maradhi kwa kutumia visaidizi, dawa na njia za kutibu. BAKIZA (2010:419) wamebainisha kwamba uganga ni uponeshaji wa wagonjwa kwa kuwapa dawa za kiasili au za kisasa.

Kabla ya  tiba ya uganga kuwepo duniani kwanza kuliumbwa maradhi (ugonjwa) na baadaye kila maradhi yaliletwa na tiba yake. Uganga ulianza tu binaadamu alipoweza kuyakabili mazingira yake kwa kutumia tiba ya uganga.  Kwa mujibu wa mafundisho ya Mtume (SAW) wanadamu wanatakiwa kujitibu na kutibu mimea na wanyama wao.  Kwa mintarafu hiyo Mtume (S.A.W) anasema “Fanyeni dawa (tiba) enyi waja wa Mwenyezi Muungu (S.W) kwani Mwenyezi Mungu hakuleta ugonjwa isipokuwa kila ugonjwa una dawa yake.’’

Pia akasema mwenye kufundishwa dawa kisha asifundishe watu wengine na watu wakaangamia kwa ugonjwa huo basi mtu huyo atakwenda jibu siku ya kiama (Imepokewa na Abuu- Daud) kwa mujibu wa hadithi hii tiba hapa inawezakuwa ya kiasili au yakisasa. Vile vile Mwenyezi Muungu anasema ‘‘*Na tunateremsha katika*

*Qur'ani yaliyo ni matibabu na rehema kwa Waumini. Wala hayawazidishii madhaalimu ila khasara''.* (17:82).

Kwa mujibu wa Bi Kihengere wa Kisiwa Panza aliyefanya mahojiano na mtafiti siku ya10/5/2016 nyumbani kwake anasema: Uganga ni miongoni mwa Kilinge kilichozoeleka visiwani Zanzibar na kilikuwepo tokea mwanadamu alipoanza kuyakabili matatizo yake na ni moja miongoni mwa vilinge vya asili. Uganga ni jadi kongwe na ya kale na yenye kurithishwa kizazi hadi kizazi. Wanajamii wengi hufanyiwa tiba hii, kwa kipindi maalumu na itategemea hali ya muwele alivyo. Hapo awali tiba hii ilikuwa ikiandaliwa kwa umakini mno kama wanajamii wanavyojiandaa katika sherehe za Idi, harusi, mwaka kogwa. Kwa kadri siku zinavyokwenda ndivyo tiba hii ya uganga inatoweka na kushuka thamani katika jamii ya Waswahili.

## 1.3 Sababu ya Kuchagua Mada

Mtafiti alitaka kuiamsha au kuizindua jamii yake kurudi katika mila, silka na desturi zao za kijadi kwa sababu hapo awali wanajamii walikuwa wakitumia uganga kuwa tiba ya asilia tangu zama na dahari, kwani kila jana inaathari kwa kesho yake. Pia kuondosha fikra potofu kuwa uganga ni uchawi na haufai na haramu katika jamii. Vile vile mtafiti ametaka kuwaelimisha wasomi wengine ili waielewe taalimu hii ya nyimbo za uganga, ikiwa ni pamoja na kupata historia yake, miiko na maadilii yake hasa katika jamii ya Wapemba.

## 1.4 Tatizo la Utafiti

Tafiti tafauti zimefanywa kuhusiana na nyimbo. Nyimbo za uganga zimeshamiri au zinatumika sana katika uganga wa jamii ya Wapemba na jamii nyingine, na tafiti

kadhaa zimefanywa kuhusiana na eneo hili. Mfano, Sengo (1995), Mlacha na Hurskarnnen (1995), Juma (2007), Haji (2011).

Sengo (1995) alizungumzia kuhusu jadi ya Waswahili katika jando na unyago anasema: Wawele huimbiwa nyimbo kama sehemu ya tiba ili wapone. Kazi hii ya Sengo imejikita zaidi kwenye muktadha wa jando. Mlacha na Hurskarnnen (1995), wakirejelea kwa Sengo, alipochambua itikadi katika jamii ya Waswahili alisema kuwa "Uganga wa jadi ni taasisi hai katika maisha ya Waswahili". Pia waligusia kuhusu ngoma ya pungwa, akasema kuwa pungwa si ngoma bali ni uganga wa shetani. Sengo aligusia zaidi uganga wa pungwa. Juma (2007), alielezea lugha iliyotumika katika nyimbo za uganga na kusema kuwa, lugha hii hutumia mafumbo inayoibua hisi kwa hadhira. Yeye alizamia zaidi katika uchambuzi wa matumizi ya lugha katika nyimbo za uganga.

Haji (2011), yeye alielezea nyimbo za uganga hutumika kupandishia shetani kichwani mwa muwele. Ingawa watafiti hawa wamejikita kwenye vipengele kadhaa vinavyohusu nyimbo za uganga, lakini hayupo mtafiti aliyeangalia kwa undani juu ya dhamira za nyimbo za uganga na hata wale waliogusia kuhusiana na nyimbo za uganga hawakushughulikia juu ya jamii ya Wapemba.

Hivyo hili ni pengo la kiutafiti na ndio maana mtafiti wa kazi hii alilazimika kufanya utafiti ili kuziba pengo la kimaarifa liloachwa na watangulizi hao. Watafiti hao wametoa mchango mkubwa katika kazi hii ya utafiti kwani mtafiti wa kazi hii, amegunduwa kilichofanywa na watangulizi hao.

## 1.5 Lengo la Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii za Waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba.

## 1.6 Madhumuni Mahsusi

1.6.1 Kuubainisha dhamira zinazopatikana katika nyimbo za uganga zinazopatika kusini Pemba.

1.6.2 Kufafanua undani wa dhamira za nyimbo za uganga zilimo katika jamii ya watu wa kusini Pemba.

1.6.3 Kufafanua vipengele vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za uganga Kusini Pemba.

## 1.7 Maswali ya Utafiti

Ili kukamilisha lengo kuu na madhumuni mahususi ya utafiti huu mtafiti aliongozwa na maswali yafuatayo:-

1.7.1 Kuna dhamira gani zinazopatikana katika nyimbo za uganga Kusini Pemba?

1.7:2 Kuna undani upi wa dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya watu wa Kusini Pemba?

1.7.3 Ni vipengele vipi vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za uganga Kusini Pemba?

## 1.8 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu umekua na umuhimu wa kuweka kumbukumbu za nyimbo za uganga ili vizazi vijavyo vizifahamu nyimbo hizo. Hii ni kwa sababu vizazi vipya vinaonekana

kuathiriwa sana na tamaduni za kimagharibi na kuona kuwa tamaduni za jadi hazina maana. Vijana wa kileo wanajishughulisha na mambo ya kishenzi na yasioyokuwa na faida kwao. Dhana hii husababishwa na vizazi kutofahamu utajiri wa fasihi simulizi uliomo katika tamaduni zao. Vile vile utawasaidia jamii kuiangazia fani ya uganga inavyosawiri shughuli za kila siku kisiasa, kiuchumi na kijamii.Mwisho, itawahamasisha wahadhiri wa vyuo vikuu, walimu, wanafunzi wa fani ya fasihi, pamoja na wasomaji wengine kufanya utafiti mwingine zaidi kuhusiana na fani hii. Pia, utafiti huu utafungua milango ya kufanya tafiti nyingine juu fani ya uganga katika jamii nyingine.

## 1.9 Vikwazo vya Utafiti

Ukusanyaji wa data mpaka utafiti ukakamilika si jambo rahisi sana. Hivyo katika kukusanya taarifa za tasnifu hii, mtafiti alipambana na vikwazo vifuatavyo:

Mosi, tatizo la muda,kwa sababu mtafiti ni muajiriwa na hajapewa likizo la kimasomo.

Pil; usafiri utafiti huu ulifanyika katika sehemu za visiwa hivyo hali ya hewa iliweza kusababisha ucheleweshaji wa ukusanyaji taarifa.

### 1.9.1 Utatuziwa Vikwazo vya Utafiti

Utatuzi wa changamoto za utafiti ni jambo muhimu sana ambalo husaidia kukamilika kwa utafiti. Katika kuhakikisha kwamba utafiti umekamilika kwa wakati mtafiti alitumia njia za kutatua changamoto hizo.

**Mosi**, kuhusu kikwazo cha muda, mtafiti alitumia muda wa usiku, wakati anaporejea kazini na siku za mapumziko kwa lengo la uandishi wa kazi yake.

**Pili,** mtafiti alitumia wakati hali ya hewa ya bahari ilipo kuwa shuwari na kusafiri ili kwenda kukusanya data kwa wanakilinge wa fani hiyo ya uganga walio ndani ya eneo la kisiwa huko Kisiwa Panza.

## 1.10 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu uchunguzi wa dhamira za nyimbo za uganga na sio nyimbo nyengine zozote, Nyimbo hizo ni zile zilizokusanywa katika eneo la Kusini Pemba la utafiti kutoka kwa watafitiwa moja kwa moja na mtafiti hakujihusisha na nyimbo zilizoandikwa vitabuni**.** Alijihusisha na dhamira na vipengele vya kifani vilivyoibua dhamira hizo. Hakujihusisha na mambo mengine yanayohusu nyimbo hizo.

## 1.11 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika katika kisiwa cha Pemba, Mkoa wa kusini Pemba, Wilaya ya Mkoani, katika vijiji vya Kisiwa Panza, Mkanyageni na Michenzani. Sababu iliyomfanya mtafiti achague maeneo hayo ni kupatikana kwa wingi na urahisi kwa wanafani hiyo ya uganga pamoja na nyimbo zao.

## 1.12 Hitimisho

Sura hii imeelezea usuli wa mada na sababu ya kuchaguwa mada. Vile vile imefafanuwa tamko la utafiti, sanjari na lengo kuu la utafiti ambalo ni kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga pamoja na malengo mahasusi ya utafiti huu. Pia maswali ya utafiti, umuhimu na vikwazo vya kiutafiti pamoja na utatuzi wake, mipaka ya utafiti sambamba na eneo la utafiti yote yaliangaliwa katika sura hii ya kwanza.

# SURA YA PILI

# UTALII WA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA

## 2.1 Utangulizi

Sura hii ilibainisha machapisho tafauti yanayohusiana na mada, maana ya utalii, kazi tangulizi, mkabala, ufafanuzi wa istilahi na mkabala wa kinadharia ambao ulimuongoza mtafiti katika kuifanikisha kazi hii.

## 2.2 Maana ya Utalii

Pons (1992), alibainisha kuwa utalii wa kazi tangulizi huhusisha kupitia nyaraka, usomaji wa machapisho yaliyoandikwa ambayo mtafiti anategemeya kupata taarifa anazotafuta kulingana na mada na malengo yake ya utafiti. Hivyo mtafiti ametalii machapisho kama vile, majarida, wavu pepe na vitabu na kusikiliza vyombo vya habari ili kupata data anazozihitaji. Pia kutalii ni namna ya usomaji kwa lengo la kupekua taaluma iliyojificha. Kwa kulielewa hili, mtafiti alilazimika kusoma vitabu, majarida, tasnifu za watafiti waliomtangulia, mitandao ili kufichua siri za watafiti tangulizi na kupata maarifa zaidi na wepesi wa kufanya utafiti huu**.**

## 2.3 Maana ya Mkabala

Wamitila (2003), anasema kuwa mkabala ni hali ya kuelezea utaratibu au njia ya kufanyia jambo fulani. Mfano mtu anapotaka kuhakiki kazi huchagua utaratibu unaomfaa katika uhakiki wake na utaratibu huo huitwa mkabala wa uhakiki.

## 2.4 Maana ya Nyimbo

Finnegan (1977) na Sengo (1978) wanasema kwamba nyimbo zilianza pale tu binaadamu alipoanza kupambana dhidi ya mazingira yake katika shughuli mbali

mbali za uzalishali mali. Naye Mwakasaka (1977) anasema kuwa kutunga nyimbo ni sanaa inayohitaji kipaji maalumu, ujuzi wa kuwasilisha mawazo kiufundi na matumizi makubwa ya picha. Pia anafafanua kwamba wakati mwingine nyimbo huambatana na vifaa vya kimuziki. Mulokozi (1987:7) anasema "Wimbo ni kila kinachoimbwa .Kwa mfano wimbo usemao,

*Jabiri mototo jaria, jabiri mototo jaria*

*Asukapo nywele zake mwana wa jinni ruhania*

*Kanipendeze kidomo na pua jamani pendo lauwa*.

Nyimbo ni aina ya sanaa katika fasihi ambayo hutumia lugha teule, sauti ya kiimbo maalum. (www.gafkosofti.com/swa/nyimbo). Mulokozi (1989) anaelezea makundi mbalimbali ya fasihi simulizi ambayo ni mazungumzo, masimulizi, maigizo (drama), ushairi (nyimbo na maghani), semi na ngomezi (tungo za ngoma). Anaelezea kuwa wimbo ni kila kinachoimbwa hivyo wimbo ni dhana pana inayojumuisha tanzu nyingi hata baadhi ya tanzu za kinathari,kama vile hadithi, huweza kuingia katika kundi la nyimbo pindi zinapoimbwa.Pia anaelezea mambo muhimu yanayotambulisha nyimbo ambyo ni muziki wa sauti wa muimbaji, muziki wa ala, maneno yanayoimbwa,hadhira inayoimbiwa na muktadha unaofungamana na wimbo huo. Mfano nyimbo huweza kuimbwa katika sherehe, uganga, harusi nakadhalika.

BAKIZA (2010:459), wao wamesema kwamba, wimbo (nyimbo) ni shairi lililobuniwa na kuimbwa kwa njia ya muziki au bila ya muziki. Aghlabu nyimbo hutumia ala za muziki kama vile ngoma. Nyimbo zinaweza kuimbwa na mtu mmoja au zaidi kutegemeana na mtindo husika.

### 2.4.1 Sifa za Nyimbo

Nyimbo huwa na sifa zifuatazo:

(a) Hutumia kiimbo au sauti maalumu

(b) Huweza kuendana na ala za sauti

(c) Huimbwa na mtu mmoja au wengi wakati mwingine nyimbo huimbwa kwa kupokezana

(d) Hutumia lugha ya mkato.

(e) Hurudia rudia maneno ili kusisitiza ujumbe uliyomo kwenye nyimbo hiyo.

### 2.4.2 Aina za Nyimbo

Nyimbo zimegawanyika kulingana na muundo na maudhui au ujumbe kama ifuatavyo:

(a) Kulingana na muundo (Mashairi na maghani).

(b) Kulingana na maudhui au ujumbe. Mulokozi (ameshatajwa)

**(i) Nyimbo za ndoa**

Nyimbo hizo huimbwa au huimbiwa bwana na bibi harusi kuwapongeza na kuwapa heko kwa kufunga ndoa ya. Aidha kuwapa wawili hao mawaidha ya kutunza familia, unyumba na kuishi pamoja kwa salama na amani.

**(ii) Nyimbo za jandoni**

Hizo ziliimbiwa vijana wa kiume walipotiwa tohara. Nyimbo hizo aghalabu zilionesha ushujaa, uvumilivu na ustahamilivu katika maisha.

**(iii) Nyimbo za hodia /wawe**

Nyimbo hizo ziliimbwa na watu wakati wakifanya kazi ili kuwatia mori, ari na bidii ya kufanya kazi pasi na kuhisi machofu haraka.

**(iv) Nyimbo za mapenzi**

Nyimbo hizo ziliimbwa kumsifu mpenzi, hasa kwa urembo au uzuri na tabia zake.

**(v) Nyimbo za kidini**

Ni nyimbo ambazo ziliimbwa kumsifu Mungu, kuomba au kutoa mafunzo ya kidini. Pia tungo hizo zilisomwa kwa jina lake rasmi la kaswida za kumsifu Mtume Muhammad (S.A.W), kutoa mawaidha, kuhimiza mema na kukataza maovu.

**(vi) Nyimbo za kimai**

Huimbwa na wavuvi au mabaharia wanaposafiri baharini.

**(vii) Nyimbo za kisiasa na za kizalendo**

Hizo huonesha uzalendo wa kusifu Taifa au Nchi. Wakati mwengine zinaweza hata zikawa zinamsifia shujaa fulani kutokana na uzalendo wake katika Taifa. Vle vile huimbwa kwa lengo la kuwasifu wanasiasa au viongozi wa kisiasa.

**(viii) Nyimbo za huzuni /mazishi /simanzi /msiba**

Hizo ni nyimbo za kuliwaza au kuwapa tanzia waliofiwaau kufikwa na majanga.

Mulokozi (ameshatajwa) amezigawa nyimbo katika makundi yafuatayo:

(i) Nyimbo za tumbuizo: Ninyimbo za furaha ziimbwazo kuwafurahisha watu kwenye matukio tafauti kama vile harusi, mwaka kogwa, sherehe za idi.

(ii) Nyimbo za bembea: Ni nyimbo za kubembelezea watoto.

(iii) Nyimbo za kingozi: Ni nyimbo za kuaga mwaka katika jamii ya waswahili.

(iv) Nyimbo za dini: Kama vile kasida za Kumsifu Mtume Muhammad (S AW), njimbo za ibada mkanisani, na zile za jadi.

(v) Nyimbo za wawe: Hizi ni nyimbo za kilimo.

(vi) Nyimbo za mbolezi: Ni njimbo za kilio au maombolezi.

(vii) Nyimbo za kimai: Ni nyimbo zinazohusu shughuli za baharini.

(viii) Nyimbo za nyiso: Hizi ni nyimbo za kivita.

(ix) Nyimbo za Taifa

(x) Nyimbo za vita: Nyimbo hizi ziliimbwa na askari wakati wa kivita.

(xi) Nyimbo za uwindaji: Nyimbo hizi huibwa na makundi ya wawindaji wakati wa shughuli zao.

(xii) Nyimbo za watoto: Hizi ni nyimbo zinazoimbwa na watoto wakati wanacheza iwe ni mchana au usiku.

(xiii) Nyimbo za kazi: Hili ni kundi kubwa la nyimbo. Karibu kila kazi ifanywayo na watu huwa na njimbo zao.

Kezilahabi (1981) ameelezea tanzu saba za nyimbo ambazo ni:

(i) Nyimbo za kuzaliwa

(ii) Nyimbo za jando na unyago

(iii) Nyimbo za harusi

(iv) Nyimbo za vita

(v) Nyimbo za kazi

(vi) Nyimbo za starehe

(vii) Nyimbo za wakati wa ngoma

Naye Mbarouk (1983) anafafanua nyimbo za watoto kisiwani Pemba katika michezo yao kama ifuatavyo:

(a) Kinyuli

(b) Kachiri

(c) Shaka mke wangu

(d) Watoto muwangapi

(e) Shasha mbio

(f) Njuguni lembwe

(g) Kitikiti

(h) Zikiri

(i) Mtoto alia

(j) Kitango male male

(k) Kitambaa change cheupe

(l) Kibuzi

(m) Chura

(n) Bamba

(o) Mbangano

(p) Hakuna gogo pumbavu

(q) Mnara wa njiwa na fagia uwanja.

Wataalamu wote hawa kutokana na mgawanyo huo wa nyimbo wameelezea nyimbo mbali mbali lakini nyimbo husika za kazi hii ambazo zinaimbwa katika uganga wa kienyeji hazikujitokeza. Ijapokuwa hazikujitokeza lakini sifa na maudhui au

umuhimu zinafanana na nyimbo hizo za makundi hayo kwani nyimbo zote zinahusu jamii husika.

### 2.4.2 Maana ya Uganga

Uganga ni elimu kuhusu tiba za magonjwa ya watu, wanyama, mimea, mwilini na rohoni jinsi ya kuzuia magonjwa na kuhusu njia ya kurudisha uzima. (SW.wikipedia .org/wiki/Tiba). Neno uganga huhusishwa na mambo ya kishirikina (uchawi na mauzauza). Hii ni kwa mujibu wa (sekenke.com>sekenke forums.ukumbi wasekenke >Afya na tiba). Ibnu Bazi (ameshatajwa) uganga ni fani au taaluma au elimu ambayo watu huitumia kutibu maradhi kwa kutumia visaidizi, dawa na njia mbali mbali za kutibu. BAKIZA (2010:419) uganga ni uponeshaji wa wagonjwa kwa kuwapa dawa za kiasili au za kisasa.

### 2.4.3 Nyimbo za Uganga

Nyimbo za uganga zilihusishwa na uponyeshaji wa wagonjwa kwa kuwapa dawa. Nyimbo hizo ziko katika makundi tafauti. Makundi hayo yamegawanyika na waganga wenyewe kutokana na aina za pepo. Kila pepo huimbiwa nyimbo zake ambazo ni tafauti na nyimbo za pepo mwengine. Nyimbo hizo hutofautiana katika uimbaji na hata uchezaji pia. Vilevile, nyimbo za uganga ni aina ya nyimbo zinazowasilishwa na waganga kwa wanajamii kwa lengo la kutolea tiba katika shughuli hiyo na kufikisha ujumbe kwa wanakilinge na jamii kwa ujumla. Mganga huimba nyimbo kwa lengo la kumwita shetani ili aweze kuelewana naye katika kilinge hicho lakini kinadharia huwa anatowa ujumbe kwa hadhira yake. Waganga wa kienyeji wanapokuwa katika uimbaji wa nyimbo huwa na utaratibu maalum

ambao wenyewe wanautumia. Huimba nyimbo zao kwa kuanza na pepo kama tulivyowapanga hapa chini katika makundi yao.

Kwa mujibu wa Bw Msambe wa Kisiwa Panza aliyehojiwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data tarehe 27 /5/2016 huko nyumbani kwake alisema, pepo katika jamii ya Waswahili wamegawika makundi kadhaa. Miongoni mwa makundi hayo ni kama yafutayo:

(a) Pepo wa shi: Huyu ni pepo ambaye anapoimbiwa nyimbo zake hutemea kwa kutumia makalio yake kwenda mbele akirudi nyuma pale alipokaa.

(b) Pepo wa umundi: Ni aina ya pepo ambao uchezaji wa huzunguka chano.

(c) Pepo wa hazingwa: Hawa ni jamii ya pepo ambao hucheza kwa mtindo wa kupiga magoti waimbiwapo nyimbo zao.

(d) Pepo wa pwani: Hawa wametwa pepo wa pwani kwa sababu uchezaji wao wanapoimbiwa nyimbo zao huashiria vitendo vya kupiga kafi.

(e) Pepo wa rubamba: Hawa hucheza kwa kusimama wima na kuweka kifimbo kwenye kwapa zao.

(f) Pepo wa n’njuguu: Ni jamii ya pepo ambao hucheza huku wamesima vile vile wakati wanapocheza hukizunguka chano kama ni mtindo wa uchezaji wao.

(g) Pepo wa tari: Ni aina ya pepo waocheza wakiwa wamezunguka duara.

(h) Pepo wa Ruhani: Ni pepo wanaocheza wakiwa wamepanga mistari miwili au wakati mwingine hutembea huku na huku kutegemea naaina ya nyimbo iliyoimbwa.

(i) Pepo wa kimasai: Hawa huhusishwa zaidi na jamii ya kimasai .Vile vile hujifunga rubega huku wakiwa wamejipamba vya kutosha vichani mwao.

(j) Pepo wa kisomali:Hawa hucheza kwa kusotezanyayo zake za miguu chini huku akienda mbele.

(k) Pepo wa kinyamwezi: Pepo hawa hucheza kwa kujinyongoa kiwiliwili akitoka juu kwenda chini.

Makundi yote haya kila moja lina nyimbo zake ambazo hutumiwa kwa kuimbwa wakati ambao mgonjwa anayetibiwa, akionekana anasumbuliwa na pepo anayehusika. Endapo Muwele alikibainika ana pepo wa ruhani au rubamba basi huimbiwa nyimbo za pepo huyo au akibainika ana pepo wa umundi, ataimbiwa nyimbo za pepo huyo, na waliobakia ni hivyo hivyo.

## 2.5 Dhana ya Dhamira

Sengo (2009) anasema dhamira ni sehemu ya maudhui na maudhui ni yale yasemwayo na kazi ya fasihi. Dhamira ya mtunzi wa asili yaweza kuwa ni mgogoro wa ndoa, maandishi yatoayo dhamira kadhaa juu ya kugongana wenyewe kwa wenyewe, viongozi wa serikali kutokusikilizana kwa vilabu vya mpira skuli na skuli nakadhalika.

Maelezo hayo ya Sengo juu ya dhana ya dhamira yametupa uelewa mkubwa juu ya kuweza kuchambua dhamira katika nyimbo za uganga. Mawazo yake yamemsaidia mtafiti kupiga hatua kubwa na kupata mwanga wa kina juu ya kuitambua dhana ya dhamira. Maelezo hayo yalimuongoza mtafiti jinsi ya kuangalia vipengele kama vile dhamira, wahusika, mazingira na lugha iliyotumika na miktadha ambayo yote kwa pamoja yalimsaidia katika kufanya utafiti huo.

## 2.6 Vipengele vya Kifani

Ili kukamilisha tasnifu hii, kuna vipengele vya kifani ambavyo husaidia kuibua dhamira kama vilivyoelezwa na wataalamu mbali mbali kama ifuatavyo:

### 2.6.1 Wahusika

Dhanna ya wahusika katika medani ya fasihi inatumika kurejelea watu, vitu, na viumbe tafauti vinavyotumiwa na mtunzi wa kazi ya fasihi, kubeba maneno, tabia na vitendo tafauti ili iwe ni kiwakilishi cha hali ya maisha ya watu katika kipindi au wakati unaohusika, kihistoria, muktadha na eneo litakalochangia kutungwa kwa kazi hiyo. Senkoro (1982) ameeleza kuwa wahusika ni watu ama viumbe waliokusudiwa wawakilishe tabia za watu katika kazi ya fasihi.

### 2.6.2 Mazingira /Mandhari

Njogu na Chimerah (1998) wanaeleza kwamba mandhari ni kipengele kimoja wapo ambacho katika kazi ya kifasihi husaidia kuibua dhamira. Inategemea muundo wa mandhari ulivyojengwa na mwandishi katika kisa anachokisimulia. Mandhari inaweza kuwa ya kidhahania au halisi, kwa mfano mazingira au mandhari ya dhahania ni kama vile, mizimuni, ujinini na mandhari halisi mfano, Baharini, Mtoni, Nyumbani, Jukwaani. Mandhari ya kazi ya fasihi inaweza kuibua dhamira kwa kuhusishwa na wahusika na matendo yao.

### 2.6.3 Lugha

Lugha ni kielelezo cha jamii na kiwakilishi cha utamaduni ambacho hubeba dhana za kiisimu kama malighafi ya jamii husika, utamaduni huweza kuelezwa kikamilifu na lugha ya jamii husika (Jilala, 2014). Vile vile Mwansoko (1996) anaielezea lugha

kama kipengele na kielelezo muhimu cha utamaduni wa jamii. Kwa maana hizo tunaweza kusema kwamba lugha ya nathari kwenye kazi za nathari au tutumbi zenye hisia zikilinganishwa na zile za ushairi na ambazo huambatana na ishara, sitiari na tamathali nyingi za usemi. Katika mtiririko wa lugha kuna mtindo wa simulizi, mtindo wa kurejelea pamoja na wamazungumzo. Kwenye Kazi ya fasihi, lugha mara nyingi ndiyo inayotumika kufikisha dhamira kwa hadhira. Ili kazi ya fasihi iwe na mvuto na mnato msanii hutumia vipengele tafauti mfano; sitiari, methali, takriri. Vipengele hivyo vikitumika vizuri huweza huibua dhamira katika kazi ya fasihi. Mfano; takriri, hutoa msisitizo wa jambo, hivyo mhakiki wa kazi ya fasihi aliweza kuibua dhamira kutokana na takriri hiyo.

## 2.7 Utalii wa kazi Tangulizi

Utalii ni usomaji wa kina au mzamo wa kutafuta ukweli wa jambo. Utalii wa kazi tangulizi ni jumla ya utalii uliofanyika ambao unalingana na mada ya utafiti husika. Omar (2012) anasema kwamba, kazi tanguluzi hutoa ujuzi au maarifa ya wanawazuoni waliowahi kufanya kazi yenye mwelekeo na lengo la utafiti. Vilevile humsaidia mtafiti kutambua mambo yepi yamefanyiwa utafiti na yepi bado. Pia kazi tangulizi ni marejeleo yenye miono na maarifa kuhusu kweli zilizopatikana huko nyuma.

Topan (1971) alieleza katika utafiti wake kwa undani muktadha wa miviga, imani na matendo kwa kuirejelea historia ya utamaduni wa jamii ya waswahili wa Mombasa. Hata hivyo, katika kazi yake Topan hakuzungumzia nyimbo za uganga kwani haikuwa miongoni mwa malengo yake. Masuala ya pungwa ni katika mila za kijadi. Kazi ya Topan ni tafauti na ya utafiti huu ambao umekusudia kukusanya na

kuchambua nyimbo za uganga wa jamii ya Wapemba, Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Mkoani jimbo la Mkoani.Kwa hivyo mtafiti wa tasnifu hii aliangalia dhamira za nyimbo za uganga ili kuziba pengo la kiutafiti lililoachwa na mtangulizi huyo.

Kezilahabi (1981) ameangalia tanzu saba tu za nyimbo ambazo ni nyimbo za kuzaliwa, za jando, za unyago, nyimbo za harusi, nyimbo za vita, nyimbo za kazi, nyimbo za starehe na nyimbo za wakati wa ngoma. Mtafiti huyu hakujishughulisha na kuangalia dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya Wapemba.Mtafiti wa kazi hii alielekea zaidi katika kuangalia dhamira za nyimbo za uganga ili kuziba pengo la kiutafiti lililoachwa na mtafiti huyo.

Sengo (1995) akizungumzia kuhusu jadi ya Waswahili katika jando na unyago anasema: Wawele huimbiwa nyimbo kama sehemu ya tiba ili wapone. Kazi hii ya Sengo imejikita zaidi kwenye muktadha wa jando lakini hakuonesha dhamira za nyimbo za uganga kwenye jamii ya Wapemba wa Kusini. Kazi hiyo ya Sengo ilimpa muongozo mkubwa mtafiti wa tasnifu hii, kwani aligusia baadhi ya vipengele vya nyimbo za uganga, ambavyo miongoni mwao ndio msingi mkuu wa tasnifu hii.

Mlacha na Hurskarnnen (1995) wakirejelea kwa Sengo, alipochambuwa itikadi katika jamii ya Waswahili alisema kuwa "uganga wa jadi ni taasisi hai katika maisha ya Waswahili". Pia aligusia kuhusu ngoma ya pungwa, akasema kuwa pungwa si ngoma bali ni uganga wa shetani. Sengo aligusia zaidi uganga wa pungwa, lakini hata hivyo hakuonekana kuchambuwa dhamira ya nyimbo za Uganga katika jamii ya Wapemba.Kazi ya Sengo ilimsaidia mtafiti, kwani kuna badhi ya nyimbo huenda zikatumika katika tasnifu hii.

*Jarida la* Africa studies Review (2005) linaelezea nyimbo katika matambiko ya Wazigua na Wazaramo. Kwa vile mtafiti huyo aliangalia nyimbo na kuchambua baadhi ya mambo yaliyopatikana katika nyimbo hizo, mtafiti wa kazi hii alipata mwelekeo mzuri katika kupeleka mbele kazi yake kwani na yeye anajishugulisha na kuangalia nyimbo, ingawa ni nyimbo za uganga na sio nyimbo za matambiko.

Juma (2007), alielezea lugha iliyotumika katika nyimbo za uganga na kusema kuwa, lugha hii hutumia mafumbo yanayoibua hisi kwa hadhira. Yeye alizamia zaidi katika uchambuzi wa matumizi ya lugha katika nyimbo alizozichambua. Kwa hivyo mtafiti wa kazi hii alifarijika sana kupitia kazi yake kwani na yeye alikwenda kujishughulisha na uchambuzi wa dhamira za nyimbo za uganga ambapo hata baadhi ya vipengele vya kifani vimetumika ikiwa ni pamoja na matumizi ya lugha katika nyimbo teule zinazopatikana kusini Pemba.

Waterman (2009) anaelezea muziki na nyimbo za matambiko ya uponyaji wa kabila la Watumbuka huko Malawi.Waponyaji wa kabila hilo hutumia ngoma na kucheza kama njia ya kuponya na kukinga magonjwa tafauti. Mponyaji hucheza muziki kwa lengo la kuituliza mizimu ili iweze kuwatambulisha chanzo cha ugonjwa na kuanza kutibu. Nyimbo hizi ni kwa ajili ya uponyaji, pia ni kama tukio la kijamii. Ingawa mtafiti huyu hakuelezea dhamira za nyimbo ya uganga katika jamii ya Wapemba, lakini alitoa mchango mkubwa katika kazi hii hasa kwa vile na yeye alionekana kugusia nyimbo ambazo alizitolea ufafanuzi wa kina.

Haji (2011) alifanya utafiti kuhusu nyimbo za uganga anasema kuwa, nyimbo za uganga hutumika kupandishia shetani kichwani mwa muwele. Pamoja na kuwa

alizungumzia nyimbo hakujihusisha na kuangalia dhamira za nyimbo za uganga hasa katika jamii za Waswahili wa Kipemba. Na kazi yake hiyo ilitoa mwanga kwa tasnifu hii kwa kuona jinsi nyimbo zinzvyofafanuliwa na mtafiti naye akapata mwigo.

Asha, A na Fatma, F (2012) wameangalia athari za uchawi katika jamii ya Wazanzibar. Katika utafiti wao wamegundua uchawi na athari zake. Lengo lao ni kutoa tiba inayotumika katika matatizo (magonjwa hayo) yanayosababishwa na uchawi. Mtafiti alifaidika sana na utalii wa kazi hii, kwani mtafiti aligundua pengo la kiutafiti waliloliacha watafiti hao, ambalo ni kuchambua dhamira zinazopatikana katika nyimbo za uganga katika jamii ya Wapemba wa kusini.

Asha (2015), amechunguza dhima za nyimbo ya ngoma ya msondo wa Pemba amegundua kuwa nyimbo za msondo zina dhima kubwa katika jamii mfano kuelimisha, kutoa burudani, ustahamilivu na kadhalika. Mtafiti alifaidika sana baada ya kutalii kazi hii na kuweza kumsaidia kwa kuangazia katika kuviangalia vipengele vya kimaudhui vitakavyo msaidia katika kuchambua dhamira zitakazopatikana katika nyimbo za uganga Kusini Pemba.

## 2.8 Mkabala wa Kinadharia

### 2.8.1 Maana ya Nadharia

Chimerah (1999), Wafula (2007) na Sengo (2009) wanasema nadharia ni wazo kuu, fikra kuu, muongozo mkuu, wa mtu au jamii wa pahala fulani, wakati fulani, kwa sababu fulani. Nadharia ni muongozo inayo muelekeza mtafiti wa kazi ya fasihi.

Nadharia inatufanya tufikiri, tusaili, tuweke tashwishi na tuone ukweli. Nadharia inatoa muangaza na kuweka wazi kilichojificha.

Nadharia ni kanuni, taratibu, sheria, muongozo, mwanga wa kukuelekeza juu ya namna jambo au kitu fulani kilivyo na kinavyo kuwa, hivyo nadharia ya utafiti ni muongozo wa kufuata wakati wa kuchambua data za utafiti, humuonesha maelezo ya kufuata katika vitendo vya utafiti. Nadhariya ni muongozo unaotoa maelekezo juu ya namna ya jambo fulani linavyopaswa kufanywa au kufanyika ili kutowa matokeo yasiyoweza kutiliwa shaka yakitaaluma kwamba ni sahihi au si sahihi, (Kothari 2008). Katika utafiti wetu tumetumia nadharia ya Semiotiki na Mwitiko wa Msomaji, ufafanuzi wa nadharia hizi ni kama ufuatao:

#### 2.8.1.1 Nadharia ya Simiotiki

Kwa mujibu wa tovuti http//www.Kristisiegel.com/theory. Htm. Simiotiki ni sayansi ya ishara, matambiko, mavazi, vyakula na utamaduni tunaoishi. Nadharia ni muongozo unaotoa maelekezo juu ya namna jambo fulani linavyopaswa kufanywa au kufanyika ili kutoa matokeo yasiyoweza kutiliwa shaka ya kitaaluma kwamba ni sahihi au si sahihi (Kothari 2008). Kwenye utafiti wetu huu tulitumia nadharia ya Simiotoki katika kuchambua data za utafiti. Simiotiki ni neno la Kiyunani lenye maana ya ishara na ambalo linatumiwa kuelezea mielekeo na makundi fulani ya kiuhakiki. Makundi hayo na mielekeo hiyo imezuka na mtindo wa kizihakiki kazi kifasihi umbao unaangalia ishara za kifasihi katik kazi hiyo. Kimsingi tunaweza kusema kuwa, hii ni nadharia inayoshughulikia na ishara na uashiriaji katika kazi ya fasihi. Wamitila (2002) akimnuku De Saussure, anafafanua kwamba ishara zinazojitokeza katika kazi ya fasihi huundwa na mtunzi kwa kuzingatia muktadhawa

jamii kiuchumi, kisiasa, kijamii na hata kiutamaduni. Chander (1992) anafafanua kwamba binaadamu ni mtengenezaji na mnyambulishaji alama tafauti za ishara ambazo huzitumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Wasanii na hadhira hutumia ubunifu wa kutafsiri zao za ishara wanazokutana nazo katika kazi mbali mbali za fasihi wanazosoma au kutazama. Nadharia hii iliasisiwa na Ferdinandi de Saussure 1857-1913 Wamitila (ameshatajwa) anasema kwamba katika lugha kuna vitu viwili navyo ni kitaja, yaani umbo ambalo alama inalichukua na kirejelee jinsi inavyowasilishwa na alama hiyo. Kwa mantiki hiyo tunaweza kusema kwamba kuna kitaja na kirejelee ambavyo mahusiano yao ni yakubuni tu kulingana na tamaduni za jamii husika.

Bathes (1994) anasema kuna mihimili mitano ambayo hutumiwa na wanadamu katika mawasiliano yao ya kila siku. Mihimili hiyo ni muhimili wa kimatukio, kihemenetiki, kiseme, kiishara, kirejelezi na kiutamaduni. Hivyo, katika kuelezea namna nadharia hii ilivyotumika katika utafiti huu tumetumia mihimili miwili tu ambayo yametumika katika kuchambulia data za utafiti huu. Nayo ni Muhimili wa kimatukio na ule wa kiishara. Mapungufu ya nadharia hii inachukuliwa kwamba ishara zote kila mahali na wakati wote zina maana. Hivyo inapuuza hali nyingine za ishara kuwa hazijabeba ujumbe wowote kama alivyosema na Griffen (1997:118) ni kweli ina hatari ya kuwa juu ya kila kitu kiasi cha kupoteza uhalisia kwa mantiki hiyo ndio mtafiti alitumia nadhari nyingine ili kuziba pengo na kupata ufanisi wa kuchambua data za utafiti huu.Nadharia hii imetumika kuchambua dhumuni mahususi la kwanza na la tatu kwa kuangalia mbinu za kisanaa zinazosaidia kuibua dhamira.

#### 2.8.1.1.1 Muhimili wa Kimatukio

Kwenye muhimili huu tuliangalia namna matukio yanavyoungana na kushonana kutokana na kuathiriana katika kazi husika. Ilizoeleka kuona wataalamu wengi wa fasihi ya Kiswahili wakihusisha dhana ya matukio na vitushi na tanzu za riwaya na tamthilia kuliko ushairi (Njogu na Chimerah 1999). Hivyo tuliona jinsi njimbo za uganga kwenye kitanzu cha ushairi jinsi matukio yalivyofikisha ujumbe kwa hadhira yake. Mfano, "**nepewa kibaba haambiwa twanga, popo wazila mauwa tondoo change**", msanii wa nyimbo hii, amemtumia mnyama popo kwa kujenga matukio yanayotendwa na wanaadamu katika maisha yao ya kila siku. Mfano, uharibifu, ukorofi, ubadhilifu wa mali za umma na unyanganyi.

#### 2.8.1.1.2 Muhimili wa Kiishara

Muhimili huu unahusishwa na jinsi ambavyo msomaji alivyogunduwa maana tafauti za kiishara katika kazi ya kifasihi (Umberto 1976) , mfano unaonekana katika nyimbo ya uganga isemayo,

*Kule pangani kwa Mwinyi*

*Moto wawaka mchana*

*Ukawambie wainzi*

*Majini yanagombana.*

Tulipoyachunguza maneno ***"pangani kwa Mwinyi, moto na Wainzi",*** tumeona yametumika kiishara yenye maana ambapo mtafiti alilazimika kuyachunguza na kuyatafakari na kuyatolea ufafanuzi. Mfano, ***moto*** huweza kuashiria ugomvi kwenye jamii na ugonvi wa majini katika muktadha wa ugangani, ***wainzi*** inamaanisha wasuluhishaji **na pangani** inaashiri makazi ya watu au majini.

Nadharia hii ilimsaidia mtafiti kuchambua lugha za ishara zilizotumika katika nyimbo teule za uganga zilizokusanywa katika jamii ya Wapemba kwa kukamilisha malengo ya utafiti wetu. Sababu ya kuchaguwa nadharia hii ni kuonyesh mbinu za kisanaa zilizotumika katika nyimbo za uganga zenye kuibua dhamira hizo.

### 2.8.2 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji

Wafula na Njogu (2007) wanasema nadharia ya Mwitiko wa Msomaji iliasisiwa na James na wenzake katika miaka ya 1960-1970. Waasisi hawa ni Wajerumani, wanaamini kuwa kazi ya fasihi inapaswa kutazamwa kwa kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji. Kwani msomaji ana uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzowefu wake, na si kutokana na uzowefu wa muandishi.

Wananadharia hao wanaeleza kuwa kazi ya fasihi inajikita katika ishara na taswira. Kutokana na ishara na taswira hizo matini za kifasihi huwa hazina maana moja bali zinakuwa na maana zaidi ya moja. Hivyo mtafiti alitumia nadharia hiyo ili kutoa tafsiri kutokana na ufahamu wake mwenyewe kulingana na muktadha wa nyimbo za uganga zilizoimbwa. Msingi mkuu wa nadharia hii ni kwamba kazi yoyote ya sanaa hurejelea kazi inayosomwa kwa tafsili ili ithibitishwe kuwa kazi hiyo inaafikiana na yale yanayokumbukwa na msomaji wa kazi ya fasihi.

Hata hivyo, hubainisha jinsi miktadha ya matini isiyohusiana moja kwa moja na maandishi inavyoweza kuhusishwa na kutangamanishwa na msomaji. Hivyo nadharia hii ilitumika kubainisha dhamira katika dhumuni mahususi la kwanza na la pili. Sababu ya kutumia nadharia hii ni kutoa kutoa dhamira za nyimbo za uganga zilizoimbwa kutokana na ufahamu wa mtafiti kulingana na muktadha wa ugangani.

## 2.9 Hitimisho

Kwa kutalii kazi tangulizi za watafiti mtafiti amepata kianzio kizuri cha utafiti wake kwa kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya waswahili: Wilaya ya Mkoani, Pemba Kusini. Pia mtafiti amejiongezea maarifa ya kuchambua dhamira zilizopatikana katika nyimbo za uganga huo. Amebaini kuwa, hakuna utafiti uliofanyika juu ya dhamira za nyimbo za uganga wa jamii ya Wapemba. Mtafiti amepata fursa muafaka ya kufanya utalii ili kuziba pengo la tatizo la utafiti huu.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Sura hii inahusu vipengele kadhaa vikiwemo sababu za kuchaguwa mbinu teule ambazo ni usaili, na mbinu shirikishi ikionesha faida na mapungufu ya mbinu hizo, uteuzi wa watafitiwa, zana au vifaa vya utafiti.

## 3.2 Kuteuwa Kundi Lengwa

Cooper (1989) anaeleza kuwa kundi lengwa ni wanachama wote au hata mtu mmoja kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Kothari (1990) Enon (1998) wanaelezea kuwa kundi lengwa ni mtu mmoja, kikundi cha watu ambao mtafiti amekusudia kuwahusisha katika utafiti wake. Walengwa waliohusishwa katika utafiti huu ni waganga, wawele, na wauguzi.

Sababu iliyomfanya mtafiti kuteuwa kundi hili, ni kubwa kila mganga na utaalamu wake hivyo kwenye fani ya uganga ni lazima upate wanakilinge wanaozifahamu nyimbo za uganga namaana zake. Pia inatosha kunipatia data zilizo sahihi katika utafiti huu.

## 3.3 Uteuzi wa Watafitiwa

Babbie (1999:205) anasema kwamba uteuzi wa watafitiwa wa utafiti ni kitendo cha kuteuwa washiriki wachache kutokana na kundi kubwa la watafitiwa, ili kupata idadi ndogo ya watafitiwa watakaotumiwa katika kutoa taarifa za utafiti.

Kothari (2004) amelibainisha hili kuwa uteuzi wa watafitiwa ni mpango wa kuchagua wawakilishi maalumu kutoka katika kundi kubwa. Uteuzi wa utafiti huu ulipatikana kwa kutumia mbinu ya uteuzi lengwa. Ni sehemu ndogo ya watafitiwa, wawakilishi wa jamii ambayo mtafiti huichaguwa ili watumike katika utafiti wake kwa sababu tu ya kuwa na sifa za kukidhi mahitaji ya utafiti.

Hivyo mtafiti huwa huru kuchagua watafitiwa wanaoweza kutoa taarifa za kutosheleza. Kwa msingi huo, utafiti huu ulishirikisha watafitiwa 15 wenye mchanganuo kama ufuatao, waganga 5: wanaume 3, na wanawake 2, wawele 6: wanaume 3 na wanawake 3, na wauguzi 4: mwanamme 1 na wanawake 3. Mgawanyo huu ni kutokana na fani hii ya uganga kushughulikiwa na wanakilinge wa kike na kiume ingawa ni kwa nadra sana.

Hata hivyo, sababu iliyotupelekeya kuteuwa watafitiwa hao ni kutokana na sifa, ujuzi, na kuwa na upeo wa kutosha katika nyimbo za uganga. Pia taarifa hizo zimepatikana katika maskani halisi ya watafitiwa. Kwa kutumia mbinu ya kudhamiria kwa watu fulani (purposive) mtafiti aliweza kuwapata watafitiwa wake katika eneo la utafiti, na kuanza kufanya nao majadiliano, katika maskani zao. Mbinu hii ilifaa sana kutumika katika utafiti huu hasa kutokana na maumbile ya utafiti huu.

### 3.4 Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ni hatua moja wapo muhimu sana katika utafiti. Kabla ya kuanza kukusanya data mtafiti alipaswa kujuwa ni aina gani ya data anazozihitaji kuzikusanya na ni kiasi gani cha upeo utakaomuwezesha kuamini kuwa data alizozikusanya zinatosha kukidhi hitaji la utafiti wake. Vile vile ukusanyaji wa data

ni namna ya kutafuta taarifa mbali mbali zeye ukweli ndani yake (Kombo na Tromp 2006). Hivyo mtafiti amebainisha aina za data alizozikusanya kwa ajili ya utafiti huu; nazo ni data za aina mbili.

### 3.4.1 Data za Awali (Msingi)

Ni zile data zinazokusanywa kwa mara ya kwanza na hivyo ni data halisi (Kothari 2004). Data hizi za msingi hazijapata kukusanywa na mtafiti mwingine kwa minajili ya utafiti kama huu ambao ulikusudiwa kufanywa kwa mara ya kwanza. Wilber (2009) anaelezea kwamba data za msingi ni aina ya data ambazo mtafiti huzikusanya kwa kutumia njia za mahojiano, usaili, uchunguzi makini na hojaji. Hizi ni data hai ambazo hazijawahi kukusanywa na mtafiti yeyote yule kwa madhumuni ya kujibu maswali ya utafiti yaliyoulizwa na utafiti huu. Data hizi zilihusu nyimbo za uganga zilkusanywa katika vijiji vya Kisiwa Panza, Michenzani na Mkanyageni vijiji vyote vipo Mkoa wa kusini Pemba.

### 3.4.2 Data za Upili

Data za upili ni zile ambazo zimekwishakusanywa na watafitiwa wengine na kuchapishwa ama kuandikwa (Kothari, 2004). Panneerselven (2004) anaeleza kwamba data ya upili ni aina ya data ambazo tayari zimeshafanyiwa kazi, hivyo mtafiti hukusanya data hizo sehemu zilizoandikwa kama vile, majarida, machapishi ya serikali, vitabu, utafiti wa tasnifuni. Kadhalika, katika utafiti huu mtafiti alikusanya data za upili kutoka katika machapisho tafauti ya waandishi. Data hizi zimesaidia kuthibitisha data za msingi na kufikia lengo la utafiti huu. Data za upili hupatikana katika maktaba kwa kupitia vitabu, makala, tasnifu, majarida, magazeti na vipeperushi. Vile vile hupatikana katika wavuti na ili kuzipata data hizo

tulilazimika kusoma machapisho tafauti katika maktaba ya chuo kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar-es Salaam, Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI), Makavazi, Chuo Kikuu cha Suza, Bakiza na Maktaba ya Chake- Chake ya Chuo Kikuu Huria Tawi la Pemba.

## 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Kothari (1990) anasema kuwa ukusanyaji data ni zoezi la awali katika utafiti, ambalo humuwezesha mtafiti kupata taarifa alizozikusanya ili kumfikisha katika madhumuni yake mahsusi ya utafiti.

Hatua ya uwasilishaji na uchambuzi wa data hauwezi kufanyika kabla ya hatua hii ya ukusanyaji wa data. Ukusanyaji wa data ni zowezi linalohitaji mbinu muafaka, bila ya matumizi ya njia stahili data sahihi za utafiti haziwezi kupatikana. Kwa hivyo, katika utafiti huu, njia tafauti za ukusanyaji wa data zimehusishwa ambazo ni kama zifuatazo.

### 3.5.1 Mbinu ya Usaili

Mulokozi (ameshatajwa) anaelezea kuwa usaili ni majibizano ya ana kwa ana (au simu, kidijitali, barua pepe) kati ya watu wawili au zaidi kwa lengo la kukusanya taarifa au maoni kuhusu suala fulani la kiutafiti lililoainishwa. Kothari (2009) anaelezea kuwa usaili ni mawasiliano ya ana kwa ana ni mbinu ambayo mtafiti huwauliza maswali watafitiwa na wakati mwingine watafitiwa hupata fursa ya kumuuliza maswali mtafiti. Potton (2000) Denzin na Lincon (2000) na Sengo (1985) wanasisitiza kuwa njia hii humsaidia mtafiti kupata mawazo, mwelekeo na uwelewa wa wahojiwa.

Tulitumia njia hii kwa sababu husaidia kuibua taarifa za siri ambazo mtafiti asingeweza kuzipata, kwa kuzingatia kwamba watu wengi hupenda kuzungumza zaidi kuliko kuandika. Vile vile mbinu hii ni rahisi kufafanuwa kama swali lililoulizwa halijaeleweka vizuri. Pia hutoa fursa ya kubadilishana mawazo kati ya mtafiti na mtafitiwa. Hata hivyo, ni mbinu inayoruhusu unyumbukaji katika muendelezo wa kuuliza maswali, huweka bayana istilahi za kiuganga ambazo zinaonekana haziwezi kueleweka kwa watu wa kawaida bila ya kupata taarifa za kina kutoka kwa wanakilinge au waganga waliosailiwa. Sambamba na hilo, ni rahisi kwa mtafiti kudhibiti uteuzi wake kwa wepesi na kwa usahihi zaidi.

Mtafiti alipata fursa ya kuzungumza na wanakilinge walioteuliwa ana kwa ana na kuwauliza maswali na kusikiliza au kurikodi. Chochote kizuri hakikosi kasoro njia hii bado ina upungufu kwani haimuwezeshi mtafiti kukusanya data kutoka kwa watafitiwa wengi kwa muda muafaka kama ilivyo njia nyingine. Upungufu huu umetufanya tutumie mbinu nyingine ya shirikishi ili kuziba mapungufu ya njia ya usaili na kuweza kupata data sahihi  pamoja na kushiriki katika fani ya uganga na kutuwezesha kupata data sahihi za utafiti huu.

### 3.5.2 Mbinu Shirikishi

Ni mbinu au hali ile ya kuungana pamoja kwa ajili ya kufanya jambo au kusaidiana katika shughuli au jambo fulani. Hii ni njia inayovutia kwa mtafiti, kwani kuna uwezekano wa kupata taarifa za moja kwa moja kutoka kwa watafitiwa.Mtafiti alishiriki katika uganga kwa kuimba nyimbo hizo ili kuweza kupata kuimba. Zainab Mbwana akimnukuu Cohen (2001) kushiriki kuna mfanya mtafiti avutiwe kukusanya taarifa za moja kwa moja kutoka kwenye tukio halisi. Mtafiti wa utafiti huu

ameshiriki katika kilinge cha uganga ili kujionea mwenyewe vitendo na mambo yanayofanyika katika shughuli hiyo sambamba na kuimba nyimbo zilizotolewa katika kilinge.

Sababu iliyotufanya tutumie njia hii ni kutokana na maaumbile ya mada yenyewe kwani nyimbo za uganga ni nyimbo ambazo hupatikana kwa watu maalum na si kwa kila mtu. Njia hii imetusaidia kupata taarifa sahihi ambazo zinaendana na malengo mahususi ya utafiti huu. Vile vile imemsaidia mtafiti kuishi na jamii ya waganga, na mtafiti alikubaliwa kuwa ni miongoni mwa mwanajamii na kuweza kukusanya data kwa urahisi.

### 3.6 Mbinu za Uchanganuzi wa Data

Uchambuzi wa data katika utafiti huu ulifanywa kwa kutumiya mbinu za uchambuzi zisizo za kitakwimu unaojulikana kwa jina la mkabala wa kimaelezo. Babbie (1999) Kothari (2008) anelezea kwamba mkabala wa kimaelezo hutoa fursa kwa mtafiti kuziainisha data zake katika makundi tafauti kulingana na mada yake ya utafiti na kisha kuzipananga kwa namna ambayo ilikuwa rahisi kwake kufanya uchambuzi wa data zake. Hii ni kutokana na utafiti wa kazi yenyewe wakati wa kuchambua nyimbo za uganga mtafiti aliwasilisha, kuchambua na kujadili taarifa zilizopatikana katika utafiti huu.

### 3.7 Vifaa vya Utafiti

Kothari (2004) anamaanisha kwamba vifaa vya utafiti ni vyombo ambavyo mtafiti huvitumia katika ukusanyaji wake wa data, hivyo data zilizohitajika katika utafiti

wetu ni zile zisizo za kiidadi. Vifaa vilivyotumika katika utafiti huu ni kama vifuatavyo:

### 3.7.1 Kalamu na Karatasi

Mulokozi (1983) anafafanua kwamba kalamu na karatasi ndio vifaa vya jadi vya utafiti na hapana shaka vitaendelea kwa miaka mingi ijayo, kwani ni vifaa rahisi na vyepesi kubebeka na kutumia. Vifaa hivi vilitumika kutokea maandalizi ya awali ya utafiti kwa ajili ya kuchukulia nukuu katika maktaba na maskanini wakati wa ukusanyaji wa data.

### 3.7.2 Ngamizi/Kompuyuta

Ni zana ambayo mtafiti aliitumia kuanzia mwanzo hadi mwisho wa utafiti wake. Ilisaidia kucharazia na kuhifadhia data za utafiti.

### 3.7.3 Shajara

TUKI (1981:253) linaeleza kuwa shajara ni kitabu kiandikwacho kumbukumbu za matukio ya mambo ya kila siku. Pia yaweza kuwa ni daftari ambalo hutumika katika kuandikia kumbukumbu za kila siku, wakati wa ukusanyaji wa data maskanini masuala ya tarehe, maeneo ya utafiti, majina ya watafitiwa na matukio tafauti yalinukuliwa kwa lengo la kurejelea wakati wa kuandika ripoti ya Utafiti.

### 3.7.4 Simu na Kirimbo

Hivi ni vifaa vilivyotumika katika kunasia sauti za watafitiwa wakati wa ukusanyaji wa data na kufanyia mawasiliano maskanini. Mtafiti alifanya mawasiliano akiwa maskanini na kirimbo kwa ajili ya kurikodia mahojiano na nyimbo za uganga.

Nyimbo hizo zilirikodiwa kwenye kilingeni wakati shughuli hiyo ilipokuwa inafanyika.

## 3.8 Maadili ya Utafiti

**Mi**oongoni mwa vitu muhimu vinavyopaswa kuzingatiwa na mtafiti yeyote ni maadili ya utafiti (Kothari, 1999). Vile vile BAKIZA(2010) inafafanua kuwa maadili ni mwenendo unaokubalika katika jamii fulani. Mtafiti alitumia maadili ya utafiti ili kupata taarifa ambazo zilitoa majibu stahiki, miongoni mwa maadili hayo ni kutunza siri za watafitiwa na kutokutoa fedha kama ni sehemu ya kupatia data. Kwa munasaba huo mambo hayo yamezingatiwa ili kuufanya utafiti huu kutoa matokea sahihi ili kuweza kuaminiwa kitaaluma. Hivyo, mtafiti amevizingatia vipengele vya kimaadili ili kupata matokeo sahihi ya utafiti huu.

## 3.9 Hitimisho

Sura hii imejadili uteuzi wa kundi lengwa, uteuzi wa watafitiwa, ukusanyaji wa data, mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchambuzi wa data, vifaa vya utafiti pamoja na maadili ya utafiti. Mbinu zote hizi zimejadiliwa na kuchambuliwa kwa lengo la kukamilisha tasnifu hii,hivyo sura ya nne inahusu uwasilishaji,uchambuzi na mjadala wa data za utafiti.

# SURA YA NNE

# UWASILISHAJI, UCHAMBUZI, NA MJADALA WA DATA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura hii imefafanua uchambuzi na uwasilishaji wa dhamira tafauti katika nyimbo za uganga Kusini Pemba.Kombo na Tromp (2006) wanasema kwamba, uwasilishaji wa data ni namna ya kuangalia data ili ziweze kueleweka vyema. Kwa maoni ya mtafiti, uchambuzi wa data ni kuchanganua na kuchunguza kwa undani data zilizopatikana katika utafiti na kuzipangilia kwa umakini kwa lengo la kuzitolea hitimisho. Katika kushughulikia surah ii mtafiti amezichambua data kwa kuangalia madhumuni mahsusi ambayo ni:

(a) Kukusanya nyimbo na kubainisha dhamira ziaazopatikana katika nyimbo za uganga.

(b) Kufafanua undani wa dhamira za nyimbo za uganga zilizomo katika jamii ya waswahili Kusini Pemba.

(c) Kufafanua vipengele vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazojitokeza katika nyimbo za uganga Kusini Pemba.

Vile vile, madhumuni hayo ya utafiti yaliongozwa na maswali ya utafiti kwa kila dhumuni moja kama inavyodhihiri hapa chini.

(a) Kuna dhamira gani zinazopatikana katika nyimbo za uganga?

(b) Kua undani upi wa dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya watu wa Kusini Pemba?

(c) Ni vipengele vipi vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazopatikana katika nyimbo za uganga Kusini Pemba?

Fauka ya hayo, mtafiti aliongozwa na nadharia ya Maneno na Ishara (Simiotiki) na Mwitiko wa Msomaji. Kwenye uwasilishaji huu wa data, data zilikusanywa maskanini na maktabani kwa madhumuni ya kuonesha dhamira za uganga Kusini Pemba.Data za maskanini ndio zilizofafanuliwa na zile za maktabani zilitumika kama ni mbinu ya kujiongezea maarifa tu.

Hivyo basi, tunaanza uchambuzi wetu kwa lengo mahususi la kwanza, nalo ni Kukusanya nyimbo na kubainisha dhamira zinazopatikana katika nyimbo za uganga Kusini Pemba. Kwa kutumia mbinu ya usaili na mbinu shirikishi mtafiti alikusanya nyimbo zilizoimbwa na wanavilinge kisha na kuzichambua kwa kutumia mkabala wa kimaelezo. Lengo hilo linaongozwa na suali lisemalo, kuna dhamira gani zinazopatikana katika nyimbo za uganga? Ni zipi hizo?

## 4.2 Uwasilishaji wa Data

Kukamilika kwa usaili na mbinu shirikishi kati ya matafiti na watafitiwa, mtafiti alipata fursa ya kushiriki kuimba nyimbo za uganga zilizoimbwa na waganga wakati wa shughuli hiyo, wasaidizi na baadhi ya wauguzi waliowahi kuhojiwa wote wamekiri na kukubali kuwa nyimbo za uganga zinatoa dhamira kwenye jamii ya waswahili wa wapemba Kusini. Dhamira zilizojitokeza katika nyimbo hizo zilizokusanywa na mtafiti Kwa mantiki hiyo, uchambuzi huo unadhihirika kwenye kudadavua data. Nyimbo zilizokusanywa zinaonekana katika viambatanisho isipokuwa hapa zimetajwa sehemu tu ya nyimbo hizo.

**Nyimbo Kule pangani kwa Mwinyi**

*Kule pangani kwa Mwinyi*

*Moto wawaka mchana*

*Ukawmbile wainzi*

*Majini yanagombana e*eee

**Giningi**

*Gingingi weee, mie sitakwenda ee x2*

*Nikilia nalilia mwarine, ugogo na uchanja*

*Bikirembwe usipokwenda, maiti kan'tanza.*

***Kati ya kungwi na mwari***

*Kati ya kungwi na mwari*

*Mwerevu ni nani*

*Nani eee X2*

*Mwerevu nani? (hurudiwa rudiwa)*

***Dade mwana jema***

*Dade mwana jema x2*

*Mambo ulotenda jana eee*

*Naleo katende tena ooooo.*

***Jabiri mtoto***

*Jabiri mtoto jariaa, walilia nini suria*

*Asukapo nywele zake mwana wa jini ruhania*

*Kanipendaza kidomo na pua*

*Jamani pendo lauwa (hurudiwa rudiwa)*

***K*ina mama**

*Kina mama usiku unakucha nini raii*

*Tunampiga komwe mchawi, tuna mpiga komwe mchawi*

*Kina mama tumemrai rai manga*

*Tume mraii raii manga tumemraii raii manga.*

*(hurudiwa rudiwa )*

Kwa hivyo nyimbo nyingine zitaonekana katika kiambatanisho na kwa hivi sasa imekuwa ni muda wa kubainisha dhamira za nyimbo zilizokusanywa kama inavyodhihiri hapa chini.

## 4.3 Dhamira ya Kusifu mtu au Kitu katika Jamii

Nyimbo za uganga zina lengo za kusifu mtu au kitu katika jamii ya Waswahili wa uswahilini. Hivyo ziimbwapo nyimbo hizo katika jamii yetu, huwa na ujumbe uliokusudiwa. Lengo hili tunalipata kwa kupitia nyimbo ya *"Giningi mie sitakwenda*" na *"kungwi na mwari*". Nyimbo hizi zina lengo la kumsifia mtu.

Nyimbo ya "*ging'ingi mie sitakwenda"*inamsifia Bikirembwe, sifa aliyosifiwa hapa ni uwezo wa kumtoa maiti aliyeshinda sehemu moja na kumpeleka sehemu nyingine kama nyimbo inavyobainisha;

*" Giningi wee, mie sitakwenda ee X2*

*Nikilia nalilia mwarine, ugogo na uchanja*

*Bikirembwe usipokwenda, maiti kan'tanza"*

Kwa mujibu wa nadharia ya Simiotiki inatufafanulia matumizi ya lugha, hivyo kuna kitaja na kitajwa. Bikirembwe ni kitaja ambapo kitajwa chake ni mkuu wa waganga

katika fani ya waganga. Hivyo watabibu wa Kusini Pemba, kwenye fani hii walikuwa wanamsifu na kumshabihisha katika mazingira ya ging'ingi, ikiwa hakushiriki au kukubali yeye katika muktadha wa fani ya tiba, basi tiba hiyo itakuwa na shida kutendeka. Na maiti ni kitaja ambacho kinarejelea muwele ambaye anafanyiwa tiba ikiwa hakwenda mwenyewe Bikirembwe au kushiriki basi hakuna mtu atakayeweza kumkabili maiti huyo. Hivyo tunaona ni jinsi gani gwiji huyu alivyosifiwa kwenye jamii ya wanakilinge. Vile vile *mwalimu na mwanafunzi* siku zote hawawi sawa. Mwalimu ni bora zaidi kuliko mwanafunzi, jambo hili linadhihirika katika nyimbo ya uganga isemayo *"Kungwi na Mwari*".

Nadhariya inazidi kutupa mwanga kwa kutumia muhimili wa kiishara kutajwa Kungwi ambapo kiashiria chake ni *Mwalimu* na Mwari kiashiria chake ni *mwanafunzi*. Mtunzi wa nyimbo hii anauliza kati ya watu hawa ni nani aliyemwerevu zaidi kushinda mwenzake? Kiuhalisia kwenye jamii zetu kungwi ndiye mwerevu kwani ndyie anayemfunda mwari. Jambo hili linadhihirika katika nyimbo ifuatayo;

*"Kati ya kungwi na mwari*

*Mwerevu nani?*

*Nani ee X2*

*Mwerevu nani? (Hurudiwa rudiwa)"*

Mtunzi alikuwa na lengo la kuuliza, akimaanisha kuiuliza jamii yake kati ya wawili hawa ni nani mwenye ujuzi zaidi? Hapa mtafiti aligunduwa kuwa, lengo la mtunzi si kutaka jibu bali aliijengea picha jamii kuona kwamba mwalimu hawezi kuwa sawa

na mwanafunzi wake, kwani waswahili kwa hekima zao wanasema, “Shikio halipwani kichwa” wakimaanisha kwamba mtangulizi katika jamii yeyote huwa kanywa maji mema hata mtoto wa kwanza kwa mzazi wake, atakuwa tafauti na mtoto wa pili na watatu kimalezi. Hata katika fani ya kilinge mganga na msaidizi wake katika fani hiyo basi mganga atakuwa ndiye mtaalamu zaidi na humshinda msaidizi kwa hekma busara na ujuzi wa mambo. Vile vile ndani ya jamii kunahitajika pawepo na mtu wa busara na hekima wa kuweza kutatua mambo yanayoweza kutokea katika jamii ili wanajamii waweze kuishi kwa amani na salama hii inatokana na kuwepo kwa wazee wanaoyakabili matatizo yakiwa ya shida au raha na ndio waswahili wakasema kuwa ukubwa ni jaa na mtu mzima kwenye jamii yake anatakikana aweze kuvumilia na kustahamili matatizo yanayosababishwa na wanajamii yake.

### 4.4 Dhamira ya Mmong’onyoko wa Maadili

Mtunzi anapotunga kazi yake ya sanaa sio ombwe linalotokana na fikra zake au hisia alizonazo bali chochote anachokitungia huwa kinatokana na jamii yake, hali hiyo hutokea kwa jamii kwa kukosekana mwenendo mwema katika jamii zetu. Katika fani ya uganga kuhusu mmong’onyoko wa maadili ni jambo lililokemewa na wasanii wa nyimbo hizo, kama anavyosema Bi Saadi wa Michezani alipoimba nyimbo yake katika kilinge kilichofanyika tarehe 1/7/2016 saa tano usiku katika nyimbo ya “**dade mwana jema**” na Bi Mkwaju katika nyimbo **“mwana msimasikio”** wanasema;

*“Dade mwana jema X2*

*Mambo ulotenda jana ee*

*Na leo katende tena.’’(hurudiwa rudiwa)*

Nyimbo hii ilituonesha dhamira hiyo, kwani katika jamii zetu kuna watu wenye kwenda kinyume na maadili watu hawa husemwa kwa kuimbiwa nyimbo na kufikishiwa ujumbe kwa hadhira. Nadharia ya mwitiko wa msomaji, msomaji huiangalia kazi ya fasihi kwa kulingana na mila na utamaduni wa msomaji, kwa hivyo nadharia hii, humpa msomaji uhuru wa kutafsiri kama aonavyo kutokana na uzoefu wake.

Kwa mtafiti alibaini kuwwa, kwenye fani ya uganga kuna baadhi ya watibabu na watibabiwa huvunja miiko ya kazi hiyo nakuweza kutoa siri za wawele au hata kuwafanyia mambo ambayo hayaendani na mila, silka, kaida na dasturi na utamaduni wa utu na ubinaadamu wa mtu, kwani mmong'onyoko wa maadili, katika jamii yeyote huwa ni kikwazo katika kujenga jamii mpya ya waswahili wa uswahilini. Ama kwa upande wa nyimbo ya Bi Mkwaju anasema;

*“Mwana n'si mashikio ee*
*Yunakioja ee*
*Kagombana na mama ee*
*Kwa jambo moja ee! (hurudiwa rudiwa*)”.

Vile vile nadharia ya mwitiko wa msomaji ilitupa fursa kuiangalia kazi ya msanii jinsi alivyoona msomaji, hivyo kwa mtafiti amebaini jinsi malezi ya mama kwa mtoto wake na kumfunda malezi bora, ambayo yatamuwezesha kuishi maisha ya umoja na mshikamano na kuweza kujitambua ama mtoto wa kike au wa kiume na jinsi mabadiliko yanayomkabili ili apambane nayo kimaisha. Sambamba na hilo, nadharia inatupeleka mbali zaidi kwa kuichunguza nyimbo hii na kuifasili kwake

kuna baadhi ya viongozi hata wakapewa ushauri wa aina gani kutoka kwa watu wa chini hawawezi kuufuata ushauri huo na kuutendea kazi na kujiona kuwa, wao ndio wao tu. Hata katika fani ya kilinge mambo haya huzusha mtafaruku kati ya mwanakilinge mmoja na kilinge chingine na kupelekea kukosekana maelewano miongoni mwao mfano, mganga wa umundi anajiona yeye ni bora kuliko mganga tari au rohani hali hii hupelekea mtafaruku mkubwa katika fani hii ya tiba ya uganga na kukosekana mashirikiano ya kiutabibu katika tiba.

### 4.5 Dhamira ya Umoja na Mshikamano

Silaha ya mnyonge ni umoja na mshikamano katika jamii. Nyimbo za uganga huimbwa kwa mantiki ya kuleta umoja na mshikamano kati ya mganga, muwele na wauguzi au jamii. Mganga humuimbia muwele wake nyimbo kwa lengo la kumpandisha shetani wake pamoja na wanakilinge wengine ili shetani apande kwenye kichwa cha muwele kwa lengo la kutoa tiba, pamoja na kuleta mashirikiano kwenye fani hiyo. Nyimbo ifuatayo inadhihirisha hilo:

*Kinga na kinga ee X2*

*Ndio moto ukawaka*

*Nenda inga ndege ee*

*Wasile mpunga*

*Mwana wa jinni basara jide milango ifungwa*".

Kuwepo na umoja na mshikamano katika jamii, wanajamii wanatakikana washiriane na washikamane katika mambo yao yote ya kijamii, kisiasa, kiuchumi na kiuamaduni. Hivyo nadharia ya mwitiko wa msomaji inatoa ishara kwamba kwenye

fani ya uganga ushirikiano na mshikamano wa wana vilinge ni jambo muhimu kwani bila ya kuwepo wawele na wauguzi kwa lengo la kumtafutia tiba muwele anayesumbuliwa na matatizo kwa kupatikana kile kisababishi (shetani) ili asemeshwe, asikilizwe na wakubaliane na mganga wake.

Pia muwele huyo hutakiwa kila kilinge kinapofanyika kuhudhuria ili kutoa ushiriki wake kwa lengo la kutoa umoja na mshikamano kwenye jamii yake na wanakilinge wezake hiyo ipo katika muktadha wa ugangani lakini kwenye mazingira yetu ya kawaida suali hili linahimizwa katika jamii kwani shida ya mmoja iwe ni ya wote kwani anapopatwa ni taatizo mtu mmoja wanajamii washikamanane na washirikiane katika kulitatua tatizo hilo.

### 4.6 Dhamira ya Kufunza

Nyimbo za uganga zinafunza jamii na wanajamii kwamba popote unapopata tatizo au unapoona shari ni vyema ukakimbia kwani shari hiyo inaweza ikakusababishia matatizo, au kwenye jamii umekosa maelewano na masikilizano na wenzake basi ni vyema ukaondoka kabla ya kutokezea maafa. Mfano nyimbo hii inasema;

*Shoka ya Mwinyi ngwachani*
*Njoo nikwambie mijambo*
*Tangu kunioa kwetu*
*Sijui kula hata nguo*
*Kama hunitaki tena ee*
*Niache hapumue jakamoyo.*

**Kiitikio: Howa howa yantetema** (hurudiwa rudiwa)

Nyimbo hii huimbiwa muwele anapowekwa utangani kwa lengo la kuitwa shetani ili aje kichwani kwa muwele na kusemeshwa na mganga kwa lengo la kufundwa ili aache matatizo. Pia tunajifunza kwa kutumia nyimbo za uganga wagombanapo ndugu wa familia moja kwa mtu wa kando si vizuri kujihusisha na ugomvi huo. Endapo utajihusisha na ugomvi huo wanaweza wakaacha kugombana wao na wakakugeukia wewe ambaye ugomvi huo haukuhusu. Nyimbo ya **Kunguu na Mwewe na wao kwa wao** zinathibitisha hayo.

*Kunguu na mwewe, mwaitwa Msuka*

*Babaenu kafu, watu wazika*

*Matanga leo, wachawanyika*

**Kiitikio: Howa howa hauradhi moyo**.

Vile vile nyimbo:

*Wao kwa wao walyana*

*Ee mie mgeni wao? (hurudiwa rudiwa).*

Nyimbo hizi zote zinaelezea juu ya ugomvi na athari zake kwa jamii na wanajamii kujiepusha na ugomvi wa aina wowote, lakini nadharia ya mwitiko wa msomaji, imempa uhuru mtafiti kuchokonoa na kubaini kuwa, ugomvi mwengine hutokana na kuvunjika kwa ndoa na kusababisha watoto kuchawanyika na kila mmoja kutafuta sehemu yake ya kuishi.

Hii inaonekana katika ulimwengu wa kawaida ama kwenye ulimwengu wa ugangani shetani hugombana kwenye kichwa cha muwele na kutaka kila mmoja atawale kwa muwele huyo, lakini kwa hekima, busara na ujuzi alionao mganga huelewana nao na

mmoja hupewa chano atakapokubaliana naye na kuchepuka kwa muwele yule na mwengine hubaki kichwani kwa muwele huyo kwa makubaliano bila ya bughudha wala tabu. Sanjari na hayo nyimbo za uganga zinatufunza kuwa huwezi kufanya kitu au jambo lolote bila kitendea kazi. Katika nyimbo hii tunaona kwamba, hata kucheza ngoma huwezi kucheza kama hapana ngoma, nyimbo isemayo *"mcheza hachezi pasi ngoma*". Nyimbo yenyewe ni hii ifuatayo:

*Nnda zangu lala na mapemaa*

*Mcheza hachezi pasi ngoma (hurudiwa rudiwa).*

Kazi ni uti mgongo wa maisha ya binaadamu, hivyo jamii yeyote inatakiwa ifanye kazi ili kujikwamua na adui njaa.

## 4.7 Dhamira ya Matabaka

Matabaka ni dhanna inayopelekea mgawanyiko katika jamii, kwa makundi ya jamii, kubaguana kwa misingi ya kidini, kipato, kabila, elimu, jinsia, rangi na mahali atokako mtu. (Sengo1987). Dhanna ya matabaka inafafanuliwa zaidi na Karl Marx kwa maelezo kuwa matabaka hutolewa pale ambapo baadhi ya wanajamii wanakuwa na kipato kikubwa zaidi kuliko wengine hasa kutokana na unyonge unaofanywa na kundi lililo na uwezo wa kifedha katika jamii dhidi ya tabaka masikini (Wamitila 2002). Vile vile nyimbo za uganga zinapoimbwa hufikisha dhamira kwa jamii yake, iachane na utabaka na kujijengea maadili mazuri. Nyimbo iliyoimbwa na mmoja wa msaidizi wa mganga inasema;

*Sitende kazi isiyo kinua mgongo*

*Nikitenda nigeuke ng'ombe niote pembe*.

Nyimbo hii huchezwa pale wawele wote pamoja na mganga wameshapandisha shetani na huvaa maleba ya aina moja na kifimbo kwapani na kuyumbayumba kulia na kushoto kwa mzunguko wa duara. Muhimili wa kimatukio kwenye nadharia ya simiotiki kweye nyimbo hii msanii amemtaja ng'ombe ni kitaja na kiashiria chake ni tabaka la wanyonge ambao hunyonywa, kudhalilishwa na kukandamizwa katika kipato. Pia kwenye nyimbo isemayo;

*Nepewa kibaba haambiwa twanga*

*Popo wazila mauwa tondoo changaaaaa*.

Nadharia ya simiotiki ilimpa mwanga mtafiti kwenye nyimbo hii kwa kutaja kibaba ni ishara ya kipimo katika jamii, lakini huwezi kutwanga kwa kutumia kibaba bali utatwanga kwa kutumia kinu na nchi. Na popo ni kitaja na kiashiria cha ukoloni ambao unazikandamiza nchi change.

Vile vile popo huyo huyo ni kiashiria cha Viongozi walafi, wizi, waroho, mafisadi, matapeli, wadhulumuji ambapo sifa na tabia hizi zinashabihishwa na mwanaadamu ambaye ni kiongozi asiyejaili maslahi ya raia zake. Kwenye jamii ya waswahili sifa hizo hazizungumzwi kwa ufakhari. Hivyo ndani ya kilinge cha uganga kunatakiwa kusiwe na matabaka, kwani kukiwa na utabaka huweza kukapelekea matatizo ya waganga, wagangwa na jamii hasa katika suala zima la kipato na kukosekana msaada wa kutoa tiba.

### 4.8 Dhamira ya Malezi

Dhanna ya malezi ni makuzi ya mtoto kufuatana na utamaduni wa jamii (Bakiza, 2010:219). Tunajifunza kupitia nyimbo za uganga kuwa mtoto aliapo

ukimbembeleza, usikae kimya kwani umuimbiapo mtoto nyimbo hujisikia faraja na anaweza kunyamaza kiurahisi kulikoni kukaa kimya ukamuangalia. Jambo hili tunalipata kupitia nyimbo ifuatayo:

*Mchombeze mwana ee X2*

*Mlezi hakimwa*

*Mchombeze mwana ee (hurudiwa rudiwa).*

Vile vile katika nyimbo isemayo;

*Ulezi uooo ulezi uooo*

*Kila siku kibaba mkononi cha mfuto*

*Ulezi uooo ulezi wa mwana wauwa*.

Nyimbo hii inatufunza kwamba, malezi ni jambo muhimu sana katika jamii, kwani ulezi unapotengenea na jamii hutengenea kuanzia ukoo hadi taifa. Na kinyume chake ulezi usipotengenea na jamii pia haitengenei.

Kwa mujibu wa nadharia ya mwitiko wa msomaji, inampa uhuru msomaji kuiangalia matini ya kazi ya fasihi kwa jinsi anavyoiona msomaji, hivyo mtafiti alipouchambuwa wimbo huu, alibaini kuwa huduma ya malezi huanza tokea mimba kutungwa kwenye tumbo la mama mpaka kuzaliwa kwa mtoto mpaka kufa kwake.

Hali hii ilipotokea kwa muwele ambaye alitakiwa apatiwe tiba na jamii yake humtafutia huduma hiyo ili na yeye ajihisi kuwa jamii yake inamjali na kumshughulikia kwa lengo la kumpa faraja na huduma kwa kumpatia mambo yanayostahiki katika maisha yake ya kila siku.

## 4.9 Dhamira ya Kuonya

Nyimbo za uganga zina dhamira ya kuionya jamii, uchambuzi wa data umetuonesha kuwa mtunzi anaionya jamii yake, hasa wanaume wanapoondoka majumbani mwao kwenda safari za mbali ni vyema kuwaachia wake zao mahitaji ya kutosha, kwasababu endapo hawatafanya hivyo wake zao wanaweza kufanya maovu kwa kisingizio cha kukosa mahitaji ya kutosha. Si wanawake wote kwamba wanaweza kufanya hivyo bali ni wachache miongoni mwao wanatafuta sababu tu ya kufanya maovu.

Hivyo msanii anazindua jamii hasa wanaume isiwape fursa wanawake hao, jambo hili tunaliona katika nyimbo ifuatayo;

*Naugee samba X2*

*Bwana hapo kenda mwirima*

*Pangoni Simba naugee (hurudiwa rudiwa*).

Vile vile tunapata onyo kwenye nyimbo isemayo;

*Bwana hapo kenda kufungwa*

*Usije ukadumba kilingeni mambongwa (hurudiwa rudiwa).*

Mtafiti alilibaini onyo jingine kwa jamii kwamba unapoaminiwa na mtu na akakupa siri yake ujue kwamba mtu huyo amejenga imani kwako, hivyo hutakiwi kuitoa siri bila ya idhini yake mwenyewe, kufanya hivyo ni kinyume cha maadili. Nadharia ya mwitiko wa msomaji huitazama kazi ya fasihi kulingana na mila, desturi na utamaduni wa msomaji, mtafiti amegunduwa ufundi wa mtunzi wa nyimbo hii kwa kufikisha ujumbe jinsi gani jamii inatakiwa kutunza siri. Hali hii ilionekana kwamba mwanamke huyu hakutakiwa kutoa siri ya kwamba mume wake kafungwa na ndio

maana aliyemwambia hakutakikana aitoe siri hii ndipo msanii aliposema ***"usije ukadumba''***akimaanisha **usije ukasema.**

**4.10 Dhamira ya Imani ya Dini.**

Kupitia nyimbo za uganga data zinaonesha kuwa dhamira ya imani ya dini ya kumtegemea Allah (S.W) na uwezo wake ni jambo lisiloepukika na ni jambo la msingi katika maisha yetu ya kila siku. Kwenye fani ya uganga hakuna jambo linaloweza kutendeka bila ya kumtaja na kutegemea uwezo wa Mwenyezi Mungu na mwanaadamu hawezi kutenda kitu chochote bila za nguvu za Muumba wake. Hali hiyo imedhihirika kwenye nyimbo isemayo;

*Muombwa Yeye Rabbana ee X2*

*Kwa usiku na mchana ee*

*Muombwa Yeye Rabbana (hurudiwa rudiwa*).

Nyimbo hii huimbiwa muwele wakati anapowekwa kwenye utanga na mganga huwaita mashetani kwa kuwatilia buhuri ili kuwahudhurisha kwenye shughuli hiyo kwa kumshukuru na kumuomba Mwenyezi Mungu ili kazi hiyo iweze kufanikiwa, mtafiti ameligunduwa hili kwa kuiangazia jamii tafitiwa kwamba kila kitu wakitendacho na wakifanyacho humtanguliza Mungu kwanza ili aweze kuwawezesha katika maombi yao na matendo yao kwenye maisha yao ya kila siku. Vile vile suala la kumuomba na kumtegemea Mungu limezidi kuwekwa wazi na wasanii kwenye nyimbo isemayo.

*Nipe ubani na moto*

*Tumuombe Molaa*

*Ubani ee na moto*

*Tumuombee Mola*

*Mola ee X 2.*

*Tumuombee ee Mola (hurudiwa rudiwa).*

Mtafiti alibaini kwenye nyimbo hii kuwa, suala la kumuomba Mwenyezi Mungu ni suala la msingi kwa kila jamii. Kwa mantiki hiyo kwenye fani ya kutibu kwa kutumia utibabu wa asili kumuomba Mwenyezi Mungu ni jambo lisiloepukika. Vile vile kwenye kutenda jambo lolote liwe la tiba au lakawaida mwanadamu anatakikana kutegemea na kuomba msaada kutoka kwa muumba wake katika maisha yake yote ya kila siku.

### 4.11 Dhamira ya Kuelimisha

Dhamira ya kuelimisha imejadiliwa na kuchambuliwa katika data zilizokusanywa, data zilionyesha kwamba nyimbo za uganga zinaelimisha jamii ya kawaida na jamii ya ulimwengu wa kilingeni. Nadharia ya mwitiko wa msomaji imempa dira mtafiti kwa kuiangazia jamii yake, kwenye ulimwengu wa kawaida tumeona kwamba mtu na jirani yake katika muktadha wa shambani waliolima wakiwa mpaka mmoja waweze kuaminiana wasichumiane mazao, kufanya hivyo, si katika tabia nzuri na jambo hilo halisemwi na wala halitajwi kiufakhari kwenye jamii ya waswahili. Jambo hili linathibitishwa kwa kutumia wimbo **“wenda wapi na ungo**” nyimbo yenyewe ni kama ifuatayo;

*Wenda wapi na ungoo*

*Huko mpakani eee*

*Kuna mbazi zangu (hurudiwa rudiwa)*

Kwa upande wa jamii ya ugangani muwele baada ya kupandisha shetani katika kichwa chake huimbiwa nyimbo ili aache bughudha na atoe salamu kwenye jamii ya wanakilinge, mfano nyimbo ya salamu inasema;

*Salaamu, salamu, salamu, salamu ni alaika*

*Majini yakija ee! Hutoa salamu ee! (hurudiwa rudiwa).*

Nyimbo hii inatuelimisha kuwa suala la kusalimiana kwa jamii yeyote na linatiliwa nguvu na wanajamii wenye wao, ingawa nyimbo hii ni ishara ya kuwataka majini kutoa salamu kwa namna wanavyojuwa wao wenyewe bali kiashiria hicho kinarejelea kwa jamii ya kusini Pemba, kwa kulipa kipa umbele kila mnapokutana kusalimiana kwani mkifanya hivyo mtajenga mapenzi na kuoneana huruma baina yenu kwenye jamii nzima. Vile vile wanakilinge walipoimba nyimbo hii kwa njia ya swali iliyosema*:*

*Kina mama usiku unakucha nini raiii*

Hadhira iliitikia kwa kujibu kwamba :

*Tumempiga komwe mchawi,*

*Tumempiga komwe mchawi*

*Kina mama tumewaraii raii manga*

**kiitikio Tumewaraii raii manga tumewaraiii manga**

Kwa mujibu wa nadharia ya mwitiko wa msomaji inamuongoza mtafiti kwa kuiangazia jamii yake na utamaduni wa jamii hiyo kwamba mwanamke alionekana ni kiumbe duni asiyeweza kushiriki katika jambo lolote la kijamii kama vile kusoma,

kushiriki katika huduma yeyote isipokuwa kubakia nyumbani na kusubiri kuolewa. Hali hii ilimfanya mtafiti kuitazama jamii yake pale akinamama hao walipojibu fumbo hilo na kuona kwamba nao wanahaki ya kushiriki katika masuala yote ya kijamii kama vile siasa , elimu, uchuumi na sio kukaa nyumbani tu kusubiri kuolewa hii ipo katika ulimwengu wa kawaida lakini kwenye ulimwengu wa kilingeni alionekana kuwa mwanamke hana sifa, hadhi,wala uwezo wa kufanya tiba ya uganga katika jamii ya waswahili kumbe jambo ambalo wanaonekana na maarifa ya ziada kuwashinda baadhi ya wanaume kwenye fani ya kilinge cha uganga .

## 4.12 Dhamira ya Maadili

Maadili ni mwenendo uliokubalika katika jamii fulani, pia ni mafunzo yanayohusu mwenendo mwema. (BAKIZA, 2010:213). Suala la maadili limedhihirika kwenye ukusanyaji na uchambuzi wa data zetu za utafiti. Wasanii wa nyimbo za uganga walipoziimba nyimbo zao zimeitaka jamii kuacha tabia mbaya na kujenga tabia njema, mwenendo na maadili bora yanayoridhisha kwa utu na ubinaadamu wa mtu. Mfano wa nyimbo inayodhihirisha hilo ni kama ifuatayo:

*Mwana mwanao ee X2*

*Mwana mwanao*

*Mimba si yako*

*Ya mjaliwao ee.*

Nyimbo hii imetowa changamoto kwa jamii, mwanamke anapopata ujauzito na huku yuko katika ndoa yake huwa yeye anatambuwa kuwa mtoto atakapozaliwa kuwa baba yake ni yule wa ndoa au ni wa nje ya ndoa ila mtoto yule baba yake ni nani? Suali hili uhakika wake anayelijuwa ni mama tu. Nadharia ya mwitiko wa msomaji

ilimpa mwanga mtafiti wa utafiti huu, kwani haya yote yanatokana na mila na tamaduni za waswahili, mtafiti ameangaza kwa jicho la yakinifu zaidi, nyimbo hii imeibuwa fumbo ambalo alikuwa akifumbwa mwanakilinge mwengine kwasababu mwanakilinge huyo alionekana kufanya tiba, swali likaulizwa ni nani aliyemfunda fani hii? Jibu la swali hili kwa mtafiti aliona ni ishara, ni ishara ya mtoto aliyezawa ndani ya ndoa lakini juu ya mazazi yake kuna walakini kuzaliwa kwake, ni yupi baba sahihi wa mtoto huyo.

Baada kuchunguza lengo mahsusi la kwanza, sasa ni muda muafaka kwa mtafiti kuliangalia lengo mahsusi la pili lisemalo *kufafanua undani wa hizo dhamira za nyimbo za uganga* linalolandana na suali la utafiti ambalo *ni kuna undani upi unaoibuliwa kwenye dhamira za nyimbo za uganga kusini Pemba?*

## 4.13 Undani wa Nyimbo za Uganga

Nyimbo za uganga zinakuwa na undani mkubwa kwenye jamii ya Waswahili, kwani kwa kawaida nyimbo hizo huimbwa kwa mafumbo na siku zote ‘fumbo mfumbie mjinga mwerevu hulitambuwa” kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa hadhira. Fani ya uganga ni tafauti na fani nyingine kwani kwenye uganga kwa mganga ni lazima kwake kuna mambo yamjuzu ayaelewe mambo hayo ni kama yafuatayo;

### 4.13.1 Siri ya Uganga

Mosi, Siri za nyimbo za uganga ni kutolea tiba, hivyo tiba hiyo ina siri , kunga na miiko yake ambayo ni muhimu kwa mganga kuelewa siku ya mwanzo wa mwaka, khadimu wake, maleba yake, Malaika na Majini wake ambao watatumika katika tiba

hizo pamoja na saa muafaka za kufanyia tiba na ajue saa za nuhusi za kila siku, mwezi hata mwaka.

**Siku ya mwanzo wa mwaka**, mtafiti aligunduwa wakati wa kuchambua data zake kwamba kwenye fani hii ni muhimu kujuwa mwaka umeingia siku gani? Mfano, Jumamosi, Jumapili, Jumatatu na nyinginezo, na ni mwaka wa nini? Mfano mwaka unaweza kuwa wau pepo, udongo, maji au moto. Hivyo tiba ya mwaka huo au siku hiyo itaambatana na ujuzi alionao fundi (mganga) wa tiba hiyo kwa kuongozwa na taalimu yake hiyo ambayo unamjuza kwake kuwa apime na achunguze kwa mujibu wa fani yake . Vile vile kuna **khadimu**, Khadimu ni neno la kiarabu lenye maana ya “Mtumishi”.

Katika fani ya uganga kuna watumishi ambao husaidia katika shughuli hiyo, watumishi hawa wako wa namna mbili. Kwanza jamii, hawa hujishughulisha kwa kushirikiana na mganga kwa lengo la kumpa muwele faraja kwa kumtafutia tiba kwa kutoa umoja na mshikamano kwa jamii. Pili, **majini**, ili tiba ya uganga ifikie lengo kuna majini ambayo hushirikishwa katika fani ya kilinge na hutoa mchango mkubwa wa kumsaka yule ambaye husababisha matatizo miongoni mwa majini hayo, kwa lengo la kutoa mashirikiano ya kutoa tiba.

Sambamba na hayo kuna **maleba** katika fani ya Uganga, maleba ni mavazi yanayovaliwa wakati wa kutolea tiba, mtabibu huvaa maleba yake rasmi na kuwataka wawele ambao wamekwisha kugangwa (wasaidizi) wavae maleba yao na wamvalishe muwele mpya maleba yake na kumuweka utangani kwa ajili ya kumpatia tiba. Pia mganga huvaa maleba wakati wa kutafuta tiba ya muwele wake

kwa siku ya kwanza anapoendewa na mtu mwenye shida ya tiba. Mfano wa nyimbo iliyoimbwa katika shughuli hii isemayo.

*Nashungira gombe nashungira X2*

*Nipe upanga na ngao*

*Nashungira gombe nashungira (hurudiwa rudiwa*)

Mtafiti alishiriki na kuona maleba aliyovaa mganga ambayo ni meupe na wawele pia walikuwa na mavazi kama hayo isipokuwa muwele (mgangwa) alivalishwa vazi jekundu lenye mchanganyiko na weupe. Kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaji mtafiti aligunduwa nyimbo hii iliimbwa kwenye hatua za mwisho za kilinge kwa dhamira ya kumpa muwele chano. Chano ambacho kilikuwa na mchanganyiko wa vitu tafauti kama vile mkate, yai, asali, muwa, pesa ya shaba, sharbati, sukariguru. Vitu vyote hivi hula wanajini waliohudhuria katika sherehe iyo na kila kitu huliwa kidogo kidogo na kila mwanajini hupewa baada ya kwisha kunawishwa mikono na kupewa chano hicho. Hata watoaji tiba wanaotumia ulimbe na utunduizi nao huwa na mavazi yao kwenye fani yao ya tiba. Mfano, daktari na muuguzi huwa na mavazi tafauti katika fani yao ya kutibu wagojwa Hospitalini.

### 4.13.2 Suluhisho

Dhamira za nyimbo za uganga zinatoa undani wa **suluhisho** kwa wanakilinge na jamii, mfano nyimbo isemayo;

*Mwache angurume ee*

*Mwache angurume ee simba*

*Hamli mwanawe urongo*

*Hamli mwanawe ee urongo X2.*

*Vile vile nyimbo:*

*Kule pangani kwa Mwinyii*

*Moto wawaka mchana*

*Ukawambile wainzii*

*Majini yanagomban*a.

Nyimbo hizi huimbiwa muwele wakati yuko katika uwanja wa kilinge, hili ni fumbo ambalo lilielekezwa kwa jamii. Nadharia ya simiotiki huelezea ishara ambazo hutoa maana tafauti za kifasihi, mtafiti alitumia ishara hizo kufafanuwa mikinzano na mivutano ya kishetani kwenye kichwa cha muwele na kila mmoja akitaka amiliki kiti hicho cha muwele.

Hali hii ilimpa hofu kubwa mtafiti na kutaka kukimbia katika kilinge hicho kwa woga na wasiwasi aliokuwa nao, lakini penye kuuliwa nyoka hapaachi ndombezi, hivyo mtafiti alitolewa shaka na wasaidizi wa mganga huyo na kuambiwa kwamba haya ni mambo ya kilinge usiogope.

Suluhisho ambalo lilitolewa kwa kutumia mganga kwa kumtaka yule pepo awache matatizo wakubaliane na kupawa mafingu yake na kuahidi kuacha shida zote zinazomthakili muwele ili aweze kupata unafuu au uzima na hapo ndipo mkomozi alipomchukua shetani kwa kumuimbia nyimbo isemayo.

*Ndoano hutiwa pinguuu* x2

*Na silesile za chuma  (hurudiwa rudiwa).*

Mtafiti alikwenda mbali zaidi kwa kuiangaza jamii yake kwamba popote kwenye mikinzano na mivutano basi suluhisho hupatikana ama kwa kuja wasuluhishaji au kwa kuelewana wao wenyewe. Hali hii ilimfanya mtafiti kubaini kuwa kuna baadhi ya wagonjwa matatizo yao yanaambatana na nuksi za watu (visababishi) na mganga kwa welewa wake na ujuzi alionao huenda kwa yule msababishaji na kuombwa mtu huyo amuachie ilia pate kumtibu na kupewa ridhaa ya kumfanyia tiba muwele huyo.

### 4.13.3 Undani wa Shukurani

Undani mwengine wa dhamira za nyimbo za uganga ni kutoa **shukrani**. Nyimbo za shukrani huimbiwa muwele kwa lengo la kutoa shukrani baada ya muwele yule kupata nafuu au uzima, shukrani hizo hupelekwa kwa Mwenyezi Mungu (s.w), mganga na kwa wauguzi. Mfano nyimbo isemayo;

*Kushakula kushashiba Alhamdulillah X2*

*Kushukuru kila upatacho ndio kazi ya mja.*

Vile vile nyimbo ya hongera inasema;

*Hongera jamani hongera*

*Hongera aa hongera*

*Na mwalimu ahongere*

*Hongera aa hongera*

*Na muwele ahongere*

*Hongera aa hongera*

*Na jamii ihongere*

*Hongera aa hongera*.

Nadharia ya mwitiko wa msomaji imempa mwanga mtafiti baada ya kuona kwa kushiriki, nyimbo hii huimbiwa muwele na kufunikwa nguo kwa lengo la kupawa chano na kutoa shukrani. Mtafiti alipata uhuru wa kuyaona mambo ya kiundani ambayo yalitendeka katika shughuli hiyo ya kiuganga baada ya mganga kumpasuwa ulimi wake na kutoa jina la pepo ambaye alikuwa akimsumbua muwele huyo, hivyo baada ya kazi yoyote ile suala la shukurani ni jambo lisiloepukika, mfano kwa msafiri anayesafiri aliyeenda sehemu ambayo haijui alipouliza na kuelekezwa na mwenyeji aliyemkuta basi hutoa ahsante kwa lengo la shukrani, hali hii ipo katika mazingira yetu ya kawaida, ingawa kwa upande wa kilingeni shukrani za pekee hupelekewa mlijuu, mganga na jamii ya wauguzi kwa kumpa faraja muwele na kujihisi kuwa nay eye ni miongoni mwa wanajamii ambaye jamii yake inamjali na kumfariji kwa kumtafutia tiba na kupata unafuu wa maradhi yake.

Tukiangazia lengo mahsusi la tatu la utafiti huu, *linasema kufafanuwa vipengele vya* ki*fani vinavyosaidia kuibua dhamira katika nyimbo za uganga* likishikamana na suali lisemalo, ni vipengele vipi vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira katika nyimbo za uganga Kusini Pemba? Vipengele hivyo vya kifani ni hivi vinavyodhihirishwa hapa chini.

## 4.14 Uchambuzi wa Vipengele Vya Kifani

### 4.14.1 Mandhari

Mandhari ni mazingira na matendo yanayofanyika katika kazi ya fasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalum. Hivyo basi mandhari ni ile elementi katika kazi ya fasihi inayomuwezesha msomaji kujua ni wapi ni lini matukio yanayowasilishwa yalitendeka.

Gills (2006) anasema kuwa mandhari ni dhana pana na jumuishi. Anaungwa mkono na Wamitila (2008) anayejumuisha dhana ya mazingira, mawanda na wakati ndani ya mandhari, kwao mandhari, si mazingira ya kijografia tu bali hurejelea masuala mengine kama vile kipindi cha matukio na mwanda wa matukio kama inavyodhirishwa na matendo ya wahusika. Mandhari huwa ni kipengele muhimu katika uchambuzi wa dhamira. Sababu ya kimsingi ni kwamba matukio katika kazi ya kifasihi na maudhui yanahusishwa na matukio hayo kutendeka mahali, wakati na katika mawanda fulani.

Nafasi ya mandhari katika kazi ya fasihi hutegemea nafasi yake katika uendelezaji wa dhamira. Mandhari hufungamanishwa na wahusika, matumizi ya lugha, matendo yao, usawiri wao wa usanii ni pamoja na hulka zao katika kukuza na kuendeleza dhamira kwani matukio ni zao la wahusika. Azimio letu ni kuangalia nyimbo za uganga au vifaa tafauti hata vikafikia kuwa viwakilishi vya ulimwengu wa wahusika wake. Mandhari yanayojitokeza katika nyimbo za Uganga ni ya kiyakinifu kwani mazingira yanayorejelewa ni mazingira yanayosawiri mazingira ya jamii tunayoishi. Mfano,

*Kule pangani kwa Mwinyi*
*Moto wawaka mchana*
*Ukawambile wainzi*
*Majini yanagombana.*

Nadharia ya Simiotiki kwa kutumia muhimili wa kiishara msomaji hugunduwa ishara tafauti zilizojitokeza kwenye kazi ya fasihi, hivyo mtafiti amebaini mazingira

ya pangoni ambapo jamii ya waswahili huamini kuwa ni sehemu inayotumika katika fani ya uganga, na kudhani kuwa ni sehemu mbaya ambayo mtu haruhusiwi kufanya shughuli yeyote ya kijamii isipokuwa ya kilinge tu.

#### 4.14.1.1 Mazingira ya Giningi

Giningi ni sehemu ambayo ikitajwa kwa wanajamii wa kusini Pemba moja kwa moja hukupeleka katika kijiji cha Chambani. Nyimbo za uganga huakisi mazingira ya giningi kama ni kitajwa kwa mujibu wa nadharia ya simiotiki na kirejeleo chake ni sehemu ambayo ina mambo tafauti ya kimazingaobwe katika muktdha wa ugangani.

Mtafiti aligunduwa kwamba giningi si sehemu nzuri kwa watu wa kawaida kwani kwenye sehemu hiyo husawiri vitisho, shida na matatizo ila kwa upande wa ulimwengu wa kawaida, giningi ni sehemu yenye mandhari maridhawa na upepo mwanana wenye kusawiri maisha ya raha mustarehe kwa watu wenye kuishi mazingira hayo. Haya yanadhihirika katika nyimbo ifuatayo;

*Watoto mwacheza ngoma ee*

*Giningi hamuna uwanja (hurudiwa rudiwa*).

#### 4.14.1.2 Mazingira ya Nyumbani

Nyimbo za uganga huakisi mazingira ya nyumbani, mandhari ambayo hudhihirishwa kwa nyimbo hii;

*Mama aliponizaa kanizaa mbio mbio*

*Akanambia kupuka, ukacheze na wenzio*.

**Kiitikio; Howa howa yantetema**.

Mtafiti amejenga picha ya mji, vijiji na vitongoji vyake kuwa suali la uzazi hufanyika kwenye mazingira hayo, msanii hakuwa na maana ya kwamba mtoto anapozaliwa tu hunyanyuka na kutembea, nadharia ya mwitiko wa msomaji, imempa uhuru msomaji kutafsiri kama aonavyo kwa kutazama mila, desturi na utamaduni wa jamii yake, hivyo katika zama hizi tulizonazo mwanadamu hutakiwa kujitafutia shughuli ambazo zitamuwezesha yeye mwenyewe kumsaidia kimaisha.

Vile vile mandhari ya vijijini na maisha ya watu hao jinsi hali zao zinavyokuwa na tabu katika makaazi, hili kwa mtafiti amelizingatia wakati nyimbo ya uganga ilipoimbwa kumuimbia muwele katika kijiji cha kisiwa Panza mganga alipoimba na kusema,

*Watu waoleee X2*

*Vibanda vifungwa wenyewe wamile.*

Kwenye nyimbo hii msanii alikuwa na maana ya kwamba vibanda vifungwa ni kitaja na kirejeleo chake kinaashiria ni mazingira ya kijijini ambapo kwenye makaazi ya watu.

#### 4.14.1.3 Mazingira ya Baharini na Porini

Wasanii wa nyimbo za uganga hujenga na kuchora picha katika fikra za kibinaadamu na kufikisha kusudio lao walilolikusudia kwa hadhira wakai nyimbo za uganga zinapoimbwa. Mfano nyimbo hii,

*Makame tukavue ngogo maji yavunda*

*Sebu ee nguo yangu ndogo kutiliwa vumba.*

Nyimbo hii imesawiri mazingira ya baharini kwani kwa wanajamii wanaoishi mazingira ya baharini ukitaja samaki ngogo, msanii ametuchorea kwa kutumia muhimili wa kimatukio alimtumia samaki ngogo kujenga matukio tafauti yatendwayo na binaadamu katika maisha yao. Mfano nyimbo hii imetuoneha tukio la mtu ambaye ni mkorofi, fatani ambapo kwa sifa hizi hawezi kutajwa kwa ufakhari kwenye jamii ya waswahili. Vile vile kwenye nyimbo *nende hauchimbe* inasema;

*Nendeuka ukanambia X2*

*Wenda nipa kuchelewa njiani*

*Nende uka ukanambia*

*Nende hauchimbe wee*

*Unyorore ee dawaa.*

Nadharia ya mwitiko wa msomaji ilimuongoza mtafiti kubaini yaliyomo kwenye nyimbo hiyo kwani kuna mganga alikuwa anataka kumfahamisha mwanafunzi wake dawa lakini kutokana na penye kilinge palikuwa pamejaa watu ikambidi mganga afiche taaluma hii mpaka watu hao walipoondoka, hali hii ilisawiri na kuakisi mazingira ambayo tiba za mitishamba hupatikana na kutumika katika jamii ya waswahili.

### 4.14.2 Matumizi ya Lugha

Kwenye kuijenga kazi yeyote ya kifasihi lugha ndio muhimili mkuu, kwani bila ya lugha itakuwa hakuna kazi ya fasihi. Watunzi walijaribu kwa kiasi kikubwa kutumia lugha za taswira katika kuzipamba kazi zao. Mtafiti wa utafiti huu amebaini lugha za kitaswira zilizotumika katika nyimbo za wanakilinge hawa kama zifuatazo:

#### 4.14.2.1 Matumizi ya Taswira

Ni picha zinazojitokeza baada ya matumizi ya semi na ishara. Matumizi mazuri ya taswira na ishara hutegemea ufundi wa mtunzi wa kuweza kuchota mambo tafauti yanayomzunguka yeye na jamii yake na pia kutoka katika historia nyingine za maisha azijuazo.

Mtafiti amebaini kuwa ndani ya nyimbo za uganga kuna nguvu kubwa ya kuganda akilini taswira hizo na kunasisha ujumbe wa mtunzi kwa hadhira yake. Hivyo, nyimbo hizo hushughulikia hisia za ndani na kuweza kumfanya msikilizaji awe na hisia, aone woga, apandwe na hasira na asikie kinyaa. Mfano nyimbo isemayo;

> *Nepewa kibaba haambiwa* twanga
>
> *Popo wazila mauwa tondoo* changa.

Nadharia ya simiotiki kwa kutumia muhimili wa kimatukio, mtunzi amemtumia popo ili kuonesha matukio ya hali ya wasiwasi ya mnyama huyu au ndege huyu jinsi anavyoharibu vitu katika jamii. Tunaelewa uharibifu wa popo tulipopiga picha ya mtu aliyeharibiwa mazao yake shambani tumeweza kujenga picha juu ya hasira aliyonayo mtu huyo. Hata hivyo popo ni kiwakilishi cha kitajwa na kiashiria chake kwenye kazi ya fasihi ni watu wenye kuhodhi mali za watu, wafedhuli, waonevu na wanyonyaji. Ama kwa upade mwingine tunaweza kusema kuwa ni mataifa ya kimagharibi yanavyozinyonya na kuzinyanyasa nchi zinazoendelea.Vile vile kuna lugha ya taswira katika nyimbo ifuatayo;

> *Makame tukavue ngogo maji yavunda*
>
> *Sebu ee nguo yangu ndogo kutiliwa vumba.*

Msanii ametumia taswira katika nyimbo hii pale aliposema maji yavunda, kwa mujibu wa nadharia ya simiotiki kwa kutumia muhimili wa kiishara mtafiti alibaini kuwa hayo ni maji ya bahari yenye kupwa na kujaa, ingawa kirejeleo chake ni jinsi muwele anavyoteseka na maradhi yanayomthakili na baadaye kupata unafuu wakati alipokwisha kufanyiwa tiba.

#### 4.14.2.2 Lugha ya Picha

Nyimbo za uganga hutumia lugha za picha ili kufikisha dhamira kwa hadhira yake. Mfano wa nyimbo "*mwana nsimasikio",* mtafiti ametumia nadharia ya simiotiki kwa kubaini kitajwa ambacho ni mwana n'simasikio ambapo kirejeleo chake ni mtu asiyesikia lolote aambiwalo.

Mtafiti amebaini kwenye zoezi la ufafanuzi wa data kuwa mtu aambiwapo jambo ni wajibu wake jambo hilo kulifikiria na kulifanyia kazi, ikiwa jambo hilo litaleta mafawafu kwa upande wake basi hana budi kulifanya na kuliacha pindi litakapomletea madhara kwake, kwani wahenga walisema ***"majuto ni mjukuu***" na **"*asiyesikia la mkuu huvunjika guu"***. Hivyo yale majuto au jaza atakayoipata ndiyo itakayompasa ajute juu ya jambo hilo au manufaa atakayoyapata atajivunia kwa manufaa hayo.

#### 4.14.2.3 Tashihisi

Ni usemi wenye kukipa sifa ya uhai kitu kisichokuwa na sifa ya uhai (Bakiza 2010:390). Naye Senkoo (1982) anfasili kuwa tashihisi ni tamathali ya usemi ambayo wakati mwingine huitwa tamathali ya binadamu. Kwenye nyimbo ya **Kunguu na Mwewe** kuna tashhisi iliyotumiwa na msanii isemayo, ***"hauradhi***

***moyo”,*** hapa umetajwa moyo ambapo moyo hauwezi kuwa radhi kwani mwenye sifa na uwezo wa kuridhika ni binaadamu, kwani ndiye anayeweza kusamehe juu ya lile jambo alilokosewa.

#### 4.14.2.4 Matumizi ya Ishara

Ni picha zinazojitokeza baada ya matumizi mbali mbali ya semi na ishara. Matumizi mazuri ya ishara hutegemea ufundi wa msanii na huweza kuchota mambo yanayomzunguka yeye na jamii yake pia hutoka katika historia na sehemu zingine za maisha ajuazo. Watunzi wa njimbo za uganga wametumia ishara kama vile **moto** unatoa ishara ya ugonvi katika jamii, pia neno **wainzi** lenye kutoa ishara ya watu wenye kutafutwa ili kule suluhu katika jamii zao.Vile vile **mchana** ni ishara ya mapambazuko yenye kuleta matumaini kwenye jamii.

#### 4.14.2.5 Chuku/ Mubalagha

Ni tamathali ambayo hutia chuku kuhusu uwezo wa viumbe tabia zao na kuhusu sifa zao kwa madhumuni ya kuchekesha na kusisitiza. Kahigi na Mugyabuso (1979) wanazidi kufafanua kwamba chuku ni mbinu ya kisanii ambapo kitu, mtu au jambo hukuzwa zaidi ya uwezo wake. Vile vile katika lugha ya kawaida watu husema kuwa mubalagha ni utiaji chumvi katika masimulizi. Katika nyimbo za uganga wasanii hutumia chuku ili kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Mtafiti alilibaini hili katika nyimbo isemayo; ***“Mama aliponizaa kanizaa mbio mbio”*** kwenye nyimbo hii hakuna uwezekano wa kiumbe kuzaliwa leo leo na kuweza kutembea hapo hapo, kwa kutumia nadharia ya mwitiko wa msomaji, mtafiti alibaini kuwa jambo hili limeibua dhamira ya kutafuta maendeleo na wanajamii kujiepusha na tabia ya uvivu.

### 4.14.3 Wahusika

Kimai na Njogu (wameshatajwa) wanasema kwamba, mashairi mengi hayana wahusika lakini mashairi ya kimasimulizi yana wahusika, wanaendelea kusema kuwa tenzi nyingi huwa zinatumia wahusika katika ujengaji na upelekaji mbele dhamira.

Nyimbo ni kipera cha utanzu wa ushairi, hivyo hutumia wahusika, mtafiti wa utafiti huu alizichunguza na alizigunduwa kuwa nyimbo za uganga huwa zikitumia wahusika ambao hutajwa ndani yake na huwakilisha matukio au matendo yanayotendwa na binaadamu katika maisha yao ya kila siku. Wahusika hao huwa ni wanyama, watu, vitu na madubwana.

#### 2.14.3.1 Wahusika Ndege

Wasanii wa nyimbo za uganga hutumia wahusika ndege ili kufikisha ujumbe kwa hadhira zao. Wahusika hao huwa ni kiwakilishi cha matendo yanayotendwa na binaadamu katika maisha yao ya kila siku, mfano “kunguu” ni kitajwa kwa mujibu wa nadharia ya simiotiki ingawa kwa kutumia muhimili wa kimatukio, ndege huyo huakisi watu wenye sifa za woga na waswahili husema “kwa shujaa kwenda kilio kwa moga kwenda kicheko” hii ina maana kwamba muhusika huyu katika nyimbo za uganga hutajwa tu, bali ni mtu mwenye kukwepa wajibu wake na majukumu katika familia. Vile vile muhusika “mwewe” ametumiwa ili kujenga tukio la mtu mkorofi, mnyakuzi katika jamii yake, hayo yamedhihirishwa katika nyimbo ya “Kunguru na Mwewe”. Pia kuna muhusika “Popo” ametumiwa na msanii ili kurejelewa matukio yanayofanywa na binaadamu katika maisha yao ya kila siku. Mtafiti aligunduwa kuwa popo kwa upande mmoja ni ndege na kwa upande mwingine ni mnyama lakini kifasihi ndege huyu hurejelea kuwa ni mtu mwenye sifa ya usaliti, hivyo huakisi

usaliti katika jamii yake. Na alisawirika katika jamii ya kilinge kuwa ni pepo mbaya asiyesikia lolote analoambiwa na hutibiwa kwa nyungu nzito yamawe na kafara kwa lengo la kumuangamiza.

#### 4.14.3.2 Muhusika Samaki

Nyimbo za uganga zinapoimbwa huwa zinatumia wahusika samaki ili kufikisha ujumbe kwa jamii, hivyo mtunzi amemtumia samaki "ngogo" katika kazi ya kifasihi na kusababisha mtafiti kuvumbuwa maana tafauti za kiishara kwa mujibu wa muhimili wa kiishara kwenye nadharia ya simiotiki. Hivyo hali hii imempa mtafiti wa utafiti huu baada ya kukusanya data aligunduwa kuwa nyimbo hiyo ilitumika kiishara ya mtu mkali mwenye sifa za kuchukuwa na kunyakuwa vitu vya watu. Ingawa kwenye fani ya uganga samaki ngogo ni jamii ya watu wenye kufanya tiba wasiopenda mashirikiano na wenzao kwa lolote na chochote.

## 4.15 Hitimisho

Kimsingi katika sura hii, mambo yaliyojadiliwa ni pamoja na dhamira katika nyimbo za uganga Kusini Pemba. Miongoni mwa dhamira zilizoibuka ni pamoja na kusifu mtu, mmong'onyoko wa maadili, umoja na mshikamano, matabaka, maadili nakadhalika. Vile vile kuna undani uliojitokeza katika tasnifu hii ni kama vile siri zilizomo katika uganga ambapo siri hizo ni pamoja na wakhadimu, siku ya mwanzo wa mwaka, saa muwafaka ya kufanyia tiba, maleba, suluhisho na shukrani.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetoa muhtasari, mapendekezo ya tafiti za baadae pamoja na hitimisho. Kwenye muhtasari sura zote za tasnifu hii imepitiwa kwa muhtasari ili kufupisha mambo yaliyoelezwa katika hitimisho, tumepitia madhumuni mahsusi ya utafiti huu, na kuonesha kwamba matokeo gani yamepatikana. Kwa upande wa mapendekezo, tumetoa mapendekezo ya tafiti za baadaye ambazo wanataaluma chipukizi wanaweza kuzifanyia kazi katika viwango kadhaa vya taaluma za umahiri na uzamivu.

## 5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu ulijikita kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii za waswahili Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba kwa kuzingatia, lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii za waswahili: Wilaya ya Mkoani – Kusini Pemba, kwa kuzingatia malengo mahsusi ambayo ni: kubainisha dhamira zinazopatika katika nyimbo za uganga Kusini Pemba, lengo hili ambalo limefungamanishwa na suali lisemalo; Kuna dhamira gani zinazopatika katika nyimbo za uganga kusini Pemba? Lengo hili lilijibiwa kwa kukusanya na kuchunguza na kufasili na kutupatia dhamira zilizodhihiri katika nyimbo hizo.

Pia lengo mahsusi la pili, ni kufafanua undani wa hizo dhamira za nyimbo za uganga ambapo lengo hilo lililandana na swali, kuna undani upi wa dhamira za nyimbo za uganga kusini Pemba? Undani ulioibuliwa katika dhamira za nyimbo za uganga

kuwa ni tiba na mambo yake, kama vile, khadimu, Malaika, majini, suluhisho na shukrani. Na mwisho lengo mahsusi la tatu limefafanu vipengele vya kifani vinavyosaidia kuibuwa dhamira katika nyimbo za uganga sanjari na suali lenye kufafanuwa, ni vipengele vipi vya kifani vinavyosaidia kuibua dhamira zinazopatikana kwenye nyimbo za uganga kusini Pemba? Jibu la suali hili ni kwamba vipengele hivyo vilivyosaidia kuibuwa dhamira ni mazingira, matumizi ya lugha na wahusika. Hivyo malengo mahsusi yote pamoja na maswali yake yamejibiwa wakati wa kuchambuwa data katika sura ya nne ya utafiti wetu.

Tasnifu hii ina sura tano. Sura ya kwanza imelitambulisha tatizo la utafiti ambalo ni kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga katika jamii ya waswahili wilaya ya Mkoani Kusini Pemba. Utambulisho huo ulibainisha ufafanuzi kuhusu usuli wa mada, sababu za kuchagua mada, tatizo la utafiti, lengo kuu na madhumuni mahsusi pamoja na maswali ya utafiti. Vile vile umuhimu wa utafiti, changamoto na utatuzi wa changamoto hizo zilivyotatuliwa, mipaka ya utafiti, eneo la utafiti na hitimisho la sura nzima.

Sura ya pili imefafanuwa maandiko tafauti yanayozungumzia mada ya utafiti, maandiko hayo, hatimaye yametumika kubainisha pengo la kimaarifa kuhusu mada yetu. Sambamba na hayo, mkabala wa kinadharia uliotumika katika utafiti huu, ni nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji  zote zilitumika katika kuchambulia data za utafiti huu.

Sura ya tatu, tumeelezea kuhusu mbinu na vifaa vilivyotumika katika utafiti huu. Njia hizo ni pamoja na kuteuwa kundi lengwa, uteuzi wa watafitiwa, ukusanyaji wa

data, njia za ukusanyaji wa data, ambazo ni njia ya usaili na shirikishi zilitumika katika ukusanyaji wa data, njia za uchambuzi wa data na vifaa vya utafiti.

Sura ya nne imejadili uwasilishaji,uchamuzi na mjadala wa data za utafiti . Sura hii imegawanyika sura tatu kutokana na malengo mahsusi yaliyomuongoza mtafiti. Imejadili dhamira za nyimbo za uganga ambazo ni dhamira ya kusifu mtu au kitu katika jamii, mmongonyoko wa maadili, undani wa dhamira hizo na vipengele vya kifani vilivyosaidia kuibua dhamira za uganga ambavyo ni; mandhari, matumizi ya lugha na wahusika.

Na sura ya tano imehitimisha kwa muhtasari utafiti wote kwa ujumla yakiwemo matokeo ya utafiti ambayo ni kubainisha siri za nyimbo za uganga ambazo ni siri, suluhisho na shukrani pia imetoa mapendekezo ambayo yanafaa kuzingatiwa kuhusu tafiti zijazo katika fani ya uganga.

## 5.3 Matokeo ya Utafiti

Mtafiti aligundua memgi katika utafiti huu wakati wa uchambuzi wa data ambapo uchambuzi huo ulitoa matokeo kama inavyodihiri hapa chini:

Mosi, mtafiti aligundua kwenye uchambuzi wa data ni kwamba katika fani ya uganga kuna siku ya mwanzo wa mwaka, khadimu ambapo wapo katika Majini, Malaika na wanajamii nao wapo wa namna mbili ambao ni wasaidizi wa mgonjwa (muwele) na wasaidizi wa mganga. Vile vile, mtafiti katika uchambuzi wake wa data, data zilitoa matokeo kwamba kuna saa za kufanyia tiba ambapo kila siku imeambatana na saa za nuhusi ambazo kwa mtabibu haijuzu kwake kumfanyia mtu tiba. Matokeo mengine aliyoyabaini mtafiti baada ya kuchambua data aligundua

kuwa kuna maleba ambayo hutumia mganga wakati wa kutafuta tiba ya mgonjwa kwani kila siku kwenye fani ya uganga ina maleba yake ya kuvaa na wakati maalumu wa muwele kuwekwa utangani huvalishwa maleba yanayolandana na aina ya tiba hiyo. Pia, mtafiti aligundua kuwa sanaajadiiya ya fani ya uganga inaanza kupungua kasi kutokanana athari za dini na mambo ya ulimbe na utunduwizi. Mwisho, matokeo mengine ni shukrani baada ya muwele na wauguzi kutoa mashirikiano katika kumtibu mgonjwa.

## 5.4 Mapendekezo ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga  katika jamii ya Waswahili, Wilaya ya Mkoani Kusini Pemba. Hivyo mambo yote yaliyojitokeza kwenye utafiti wetu yanatokana na imani za jamii husika. Utafiti ulijikita katika kuchunguza dhamira za nyimbo za uganga.Kwa ujumla nyimbo za uganga katika tasnifu hii zimechambuliwa kwa kuongozwa ni nadharia ya Simiotiki na Mwitiko wa Msomaji.

Mtafiti amependekeza tafiti nyingine zifanyike kwa kuiangazia fani hii ya uganga kwenye vipengele vya Misamiati inayotumika katika fani ya uganga, nyungu na Chano kwenye fani ya uganga.

## 5.5 Hitimisho

Sura hii imeeleza kwa ufupi mambo yote yaliojadiliwa katika tasnifu hii. Mambo yaliyotafitiwa na mtafiti wakati wa ukusanyaji wa data maskanini, katika nyimbo zenyewe na wakati wa uchanganuzi.

Mapendekezo ya utafiti yametolewa ili kuwaongoza watafiti wajao wapate kujua pa kuanzia katika fani hii ya uganga.

Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itakuwa chachu ya kuwachangia wanawazuoni waliopo na wajao katika kuzamia zaidi utanzu huu wa uganga ili kuweka bayana hazina iliyomo kwenye fani hii na kufanyiwa utafiti kama zilivyo tanzu nyengine za sanaa jadiiya.

Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itafunguwa ukurasa mpya na kuweza kuruka vikwazo au kuvunja fikra potofu ya kuwa uganga ni uchawi. Mtafiti anaamini kuwa tasnifu hii itatoa mwanga mpya na nzuri wa kuithamini na kuipekuwa lulu hii adhimu katika midali ya tanzu za fasihi simulizi.

# MAREJELEO

Ali, A. na Mohd, F. (2012). Athari za Uchawi kwa jamii ya Wazanzibar: (Tasnifu ya shahada ya kwanza), Chuo Kikuu Chukwani Zanzibar (Haijachapishwa). Zanzibar, Tanzania.

Adam, O. A. (2014). Kuchunguza dhamira za kijamii na kiutamaduni, Tasnifu ya Phd Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Dar es Salaam, Tanzania.

*African Studies Review,* (2005). Retrived, April 2, 2010, From Muse. jhu.e/journals/Africanstudies review/48.3gerr-hart-pdf, similar.

Babbie, (1999). *The Basics of Social Research*. Belmolt: Wadswworth Publishing Companity.

BAKIZA, (2010). *Kamusi la Kiswahili Fasaha,* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Bathes, R. (1994*). The Simiotic Challenge Berkely*: Califonia: University of Califonia Press.

Chandler, D. (1992). *Semiotics: The Basics*, London: Routledge Presss.

Cohen, L. na Keith, M. (2001). *Research Methodology Education*, Dar es Salaam: London Routlege Farmer.

Copper, H. (1989). *White Plans*, New York; Longman.

Enon, J. (1998). *Educational Research Statistics & Measurement*: Makerere University Uganda.

Fennegan, R. (1970). *Oral Litrature in Africa*. Nairobi: University.

Fennegan, R. (1977). *0ral Litrature in Africa*. Clarandon : Oxford University Press.

Gills, R. (2006). *Mastering English literature*, Toleo la tatu, Houndmills: Palgrave Macmillan.

Haji, H. G. (2011). Mitindo ya Nyimbo za Uganga wa Pepo. (Tasnifu ya shahada ya Uzamili) UDOM (Haijachapishwa). Dodoma, Tanzania.

Ibni Bazi, (1982). *Jarida*. Hadhramaut: Saud Arabia.

Jilala, H. (2014). Athari za kiutamaduni katika Tafsiri: Mfano kutoka katika Matini za Kitalii katika Makumbusho ya Tanzania.Tasnifu ya Uzamivu (Phd) (Haijachapshwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salam. Dar es Salam, Tanzania.

Juma, S. (2007). Matumizi ya Lugha Katika Nyimbo za Matumizi ya Uganga. (Tasnifu ya shahada ya kwanza), Chuo Kikuu Cha Taifa Cha Zanzibar (Haijachapishwa). Zanzibar, Tanzania.

Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es Salam: Tanzania Publishing House.

Kezilahabi, E. (1981). *Ushairi na Nyimbo katika utamaduni Wetu*. Katika Omary C. K. na Mvungi, M. *Urithi wa utamaduni wetu*, (UK 119 – 137) DRS.TPH.

Kombo, D. na Tromp, D. (2006*). Proposal and Thesis Writing- an Introduction*. Nairobi: Pauliners Publications Africa.

Kothari, C. R. (1990). *Research Methodology: Methods and Techniques*, New Delhi. India. New Age International Publication Ltd.

Kothari, C. R. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques, (2nd ed)* New Delhi: New Age International Publication Africa.

Kothari, C. R. (2008). *Research Methodology*: *Methods and Techniques (2nd ed*) New Delhi: New Age International Publisher ltd.

Mbarouk, J. (1983). *Matumizi ya Lugha katika Nyimbo za Watoto,* (Tasnifu MA Kiswahili ya Fasihi) Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mlacha, S. K. na Hurskaine, A. (1995). *Lugha, Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Moh'd, A. (2015). *Nyimbo za Ngoma za msondo wa Pemba* (Tasnifu ya M.A ya Kiswahili, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Muhammed, A. S. (1998). *Swafwat – Tafsiri Quran*, Maktabat Albuht Wadirez At-Sarbiyah.

Mulokozi, M. M. (1983). *Utafiti wa Fasihi Simulizi*, Katika Makala ya Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili 111, Fasihi. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi:* Katika Mulika, Jarida la TUKI Juz. Na. 21 Dar es Salam.

Mwakasaka, C. S. (1977). *The Oral literature of Banyakyusa*, (MA-Dissertation) Unirversity of Dar es Salam.

Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri Nadharia na Mbinu*, Dar es Salam: TUKI.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi. Nadharia na Mbinu*, Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). (*1998), Culture, Perfomance and Identity*: Path of Communication in Kenya, Twaweza Communication Limited, Nairobi.

Omar, S. (2012). *Mulika, NO.31*, *Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili*, Dar es Salam: Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Omari, C. K. na Mvungi, M. (1981). *Mitaala ya lugha na Fasihi:* Na 9,*Urithi wa Utamaduni Wetu*, Dar es Salam: TPH.

Penneerselvan, R. (2004*). Research Methodology*. New Delhi: PHI learning Private Ltd.

Pons, V. (1992). *Introduction to Social Research*: Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Qablaan, O. N. (2004). Minnatu Rrahman: Saud Arabia

Senkoro, F. (1982). *Fasihi,* Dar es Salaam: Press and Publicity Centre Dar es Salaam.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi Nadharia na Tahakiki*, Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Sengo,T. Y. S. M. (1978). *Kudidimizwa kwa Fasihi na Mkoloni, Taamuli ya Fasihi*: *Nadharia, Mtazamo wa mbinu za Utafiti katika Fasihi Simulizi*. TUKI, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sengo, T. Y. S. M. (1985). The Indian Ocean Complex and The Kiswahili Folkrole: The case of Zanzibarian Tale Performance, A Phd, Thesis Submitted At The Khartoum University. Khartoum, Sudan.

Sengo, T. Y. S. M. (1995). *Itikadi za Waswahili*, Katika Mlacha na Huriskernnen (1995), Lugha Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili.(Uk 37-43) TUKI na Helsinki DAAC.

Sengo, T. Y. S. M. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: AERA Kisahili Researcher Products.

Taasisi ya Elimu, (1996). *Kiswahili kidato cha nne*, Dar es Salam: Oxford University Press.

Taasisi ya Ukuzaji Mitaala, (1993). *Kiswahili na Vyuo*, Dar es Salam: Kiwanda cha Uchapishaji Tanzania.

TATAKI, (HT), (Mhariri, Mulokozi), *Nyimbo za Kumbi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salam.

Topan, F. M. (1971). *Uchambuzi wa Maandishi ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Oxford University Press.

Urithi wa Utamaduni Wetu (uk 119-137), Dar es Salam. TPH.

Umberto, E. (1976). *A theory of semiotics*. Bloomington: India Univesity Press.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia na Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyata Foundation.

Wahidi, A. (1998). *Swarm –Al-Battar*, Saudia Arabia –Misri.

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Kiswahili Istilahi na Nadharia*, Nairobi: Focus Publicatoins Ltd.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakik*i *wa Fasihi*: *Misingi na Vipengele Vyake*, Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi*: *Misingi na Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide Muwa Publishers.

Wamitila, K. na Balisidiya, M. (1979). *Utafiti, Mbinu za Ukusanyaji Fasihi Simulizi*, Hatma yake Lugha yetu. Dar es Salaam: BAKITA.

Waterman, C. (2009). *African Music Microsofr Student 2009: DVD.Redmon* .W.A: Microsoft® Corporations (2008).

Sw,wikipedia.org/wiki/tiba iliyopakuliwa tarehe 1/3/2016 mchana saa 7:48.

www.gafkosoft. com/swe/ nyimbo iliyopakuliwa tarehe 16/5/2016 usiku saa 4:30.

www.shuledirect.co.tz/notes/review-no iliyopakuliwa tarehe 4/6/2016 saa 6;15 usiku.

# VIAMBATANISHI

## Kiambatanishi 1: Mwongozo wa Maswali ya Utafiti na Maskanini kwa Watafitiwa

1. Ni lipi lengo kuu la nyimbo za uganga?

   ………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………….

2. Kuna dhamira gani zinazopatikana katika nyimbo za uganga?..........................

   ………………………………………………………………………………………

   ……………………………………………………………………………………….

3. Jamii inaweza kuelimika kwa kutumia nyimbo za uganga?..............................

   ………………………………………..………………………………………

   ……………………………………………………………………….…………….

4. Kuna maadili gani yanayopatikana katika nyimbo za uganga……………………

   ……………………………………………………..……………………………

   ……………………………………………………………………………………..

   ………………………………………………..……………………………

5. Kwa kutumia nyimbo za uganga jamii inaweza kujijenga katika maadili gani bora?.............................................................................................................

   ………………………………………………………………………………………

6. Je, nyimbo za uganga zinaeleza undani upi katika jamii ya Wapemba?……….

……………..………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………..

7. Je, nyimbo hizi huimbiwa nani? Kwa lengo lipi?..............................................

………………………………………………………………………..……………

………………………………………………………………………………..…...

8. Na muimbaji huwa nani? Kwanini?...................................................................

………………………………………...…………………………………………

………………………………………………………………………………………..

9. Je, nyimbo hizo hasa huimbwa katika mazingira gani?......................................

………………………………………………………………………..………

………………………………………………………………………………………..

**Kiambatanishi 2: Nyimboza Uganga**

**Nyimbo Kule pangani.**

Kule Pangani kwa Mwinyi

Moto wawaka mchana

Ukawambile wainzi

Majini yanagombana.

**Nyimbo Giningi.**

Giningi wee mie sitakwenda ee X2

Nikilia nalilia mwarine ugogo na uchanja

Bikirembwe usiokwenda maiti kan’tanza.

**Nyimbo Kati ya kungwi na mwari.**

Kati ya kungwi na mwari

Mwerevu ni nani?

Mwerevu nani? (hurudiwa rudiwa).

**Nyimbo Dade.**

Dade mwana jema x 2

Mambo ulotenda jana ee

Naleo katende tena ee .

**Nyimbo Mwana nsimashikio.**

Mwana msimashikio ee

Yunakioja ee

Kagombana na mama ee

Kwa jambo moja ee (hurudiwa rudiwa)

**Nyimbo Kinga na kinga.**

Kinga na kinga ee , kinga na kinga ee

Ndio moto ukawaka,

Nenda inga ndege ee

Wasile mpunga mwana wa jini basara jide milango yafunwa.

**Nyimbo Shoka ya Mwinyi Ngwachani.**

Shoka ya Mwinyi ngwachni ,njoo nikwambie mijambo

Tangu kunioa kwetu ,sijui kula hata nguo

Kama hunitaki tena niache ,haumue jaka moyo.

**Nyimbo Kunguu na Mwewe.**

Kunguu na Mwewe mwaitwa Msuka

Babaenu kafu watu wazika

Matanga leo wachawanyika

KIITIKIO. Howa howa haurai moyo.

**Nyimbo Wao kwa wao.**

Wao kwa wao walyana

Ee mie mgeni wao eee

Wao kwa wao walyana. (hurudiwa rudiwa).

**Nyimbo Nnda zangu lala**

Nnda zangu lala na mapema

Mheza hachezi pasi na ngoma (hurudiwa  rudiwa)

**Nyimbo  Sitende**

Sitende kazi isiyo kinua mgongo

Nikitenda nigeuke ngombe niote pembe.

**Nyimbo Nepewa kibaba**

Nepewa kibaba haambiwa twanga

Popo azila mauwa tondoo changa

**Nyimbo Mchombeze mwana**

Mchombeze mwana  ee

Mlezi hakimwa

Mchombeze mwana  ee .

Ulezi uoo  ulezi uoo

Kila siku kibaba mkononi cha mfuto

Ulezi uoo ulezi wa mwana wauwa.

**Nyimbo  Bwana hapo kenda mwilima**

Bwana hapo kenda mwilima

Pangoni Simba na ugee

Bwana hapo kenda kufungwa

Usije ukadumba kilingeni mambogwa.

**Nyimbo Muombwa**

Muombwa ee Rabbana X2

Kwa usiku na mchana

Muombwa ee Rabbana.

Nipe ubani na moto tumuombe Molaa

Ubani ee na moto tumuombe Mola

Mola ee X2

Tumuombe Mola ee

**Nyimbo Wenda wapi na ungo**

Wenda wapi na ungo , huko mpakani ee

Kuna mbaazi zangu

Salamu,salamu,salamu, salamu ni alaika

Majini yakija ee hutoa salamu ee

**Nyimbo Mwana mwanao**

Mwana mwao ee ,mwana mwanao

Mimba si yako yamjaliwao ee

**Nyimbo Nashungira gombe**

Nashungira gombe nashungira x2

Nipe upanga na ngao

Nashungira gombe nashungira

**Nyimbo Mwache angurume**

Mwache angurume ee mwache angurumee simba

Hamli mwanawe urongo

Hamli mwanaee urongo.

**Nyimbo Watu wa olee**

Watu wa Ole ee X2

Vibanda vifungwa wenyewe wamile

Nendeuka ukanambia X2

Wendanipa kuchelewa njiani

Nendeuka ukanambia

Nende hauchimbe wee unyorore ee dawa.

**Nyimbo Mama aliponozaa**

Mama aliponizaa kanizaa mbioo mbioo

Akanambia kupuka ukucheze na wenzio

Watota mwacheza ngoma ee giningi hakuna uwanja.